# MITINDO NA MAUDHUI KATIKA UCHANGANUZI WA VIBONZO KWENYE GAZETI LA TAIFA LEO

**NA**

**DAMARICE ACHIEN'G OTUOMA**
**C50/84015/2012**

**TASNIFU HII IMEWASILISHWA KAMA SEHEMU YA BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI KATIKA KISWAHILI**

**IDARA YA KISWAHILI NA LUGHA NYINGINE ZA KIAFRIKA**
**KITIVO CHA SANAA NA SAYANSI ZA KIJAMII**
**CHUO KIKUU CHA NAIROBI**

**©2015**

## IKIRARI

Tasnifu hii ni kazi yangu asili na haijawahi kuwasilishwa katika chuo kingine ili kutuzwa shahada. Hakuna ruhusa ya kunakili sehemu yoyote bila idhini ya mwandishi au Chuo Kikuu cha Nairobi.

Damarice Achieng' Otuoma Sahihi--------------------Tarehe ---------------------

Tasnifu hii imetolewa kwa minajili ya kutahiniwa kwa idhini yetu tukiwa wasimamizi walioteuliwa na Chuo Kikuu cha Nairobi.

Prof. John Habwe Sahihi------------------- Tarehe--------------------

Ms. Mary Ndung'u Sahihi----------------------Tarehe------------------

# SHUKRANI

Nawashukuru wote walionisaidia kwa njia moja au nyingine.  Shukrani jazila kwa walimu, marafiki na wasomi walionitia shime na kunihamasisha kuikamilisha kazi hii na naamini ni muhimu kwangu. Kwanza kabisa ni Prof. John Habwe, Ms Mary Ndung'u , Dkt. P.I. Iribe Mwangi, na Bi. Musungu, mwalimu wangu wa kipekee aliyenipa mwelekeo kutoka shule ya Upili hadi sasa hajaacha kunipa nasaha.

Shukrani jazila kwa familia yangu walio nitia moyo kuendelea na usomi huu hadi nikafika hapa mahali nimefika. Kwa mpendwa mama Millicent Orege, Mungu azidi kupa maisha marefu kwa kuwa bila wewe kunitia moyo kila wakati nisingalimaliza kazi hii hivi leo. Ahsante sana.

Kuandikwa na kukamilika katika tasnifu hii kusingefikiwa pasi na msaada mkubwa wa wakutubi wa maktaba za vyuo vikuu; Chuo Kikuu cha Nairobi; Chuo Kikuu cha Maseno na Shule ya Upili Ya Wavulana-Kisumu na Kenya Library Services.

Mwisho, nashukuru Mwenyezi Mungu kunipa afya njema wakati huo wa utafiti huu hadi tamati.

# TABARUKU

Kwa mwanangu mpendwa Kwe Rawinyo, na "*baba*" Eng. Carey Orege, nashukuru kwa uwezo wako wakunionyesha njia ya elimu, na wewe ni jagina kwangu.

# IKISIRI

Katika utafiti huu tunalenga kuchanganua vibonzo katika gazeti la Taifa Leo. Matumizi ya mikakati ya vibonzo katika diskosi huweza kuzua utata katika kufasiri ujumbe ulionuiwa kumfikia msomaji. Tamko la msemaji au mwandishi fulani huweza kufasiriwa na msomaji kwa njia mbalimbali hasa wanapotumia vibonzo kuwasilisha ujumbe wao. Hali kama hii huibua hisia mbalimbali kulingana na ujumbe ulioko pale na hata kutatua mawasiliano. Utafiti huu ulinuiwa kubaini jinsi ambavyo vibonzo vinavyodhihirika katika kuleta dhana ya Ugatuzi kwenye gazeti la Taifa Leo. Vilevile utafiti huu umenuiwa kuonyesha jinsi mikakati hiyo inavyoathiri ufasiri wa ujumbe unaodhamiriwa na mwandishi wa vibonzo; malengo ya utafiti huu ni kuchanganua vibonzo vinavyobeba maudhui ya Ugatuzi, kuchunguza mbinu ya lugha inayopendelewa sana katika kuwasilishavibonzo hivyo na kuchanganua mitindo ya lugha inayotumika katika utunzi wa vibonzo hivyo. Nadharia ya Utambulisho/ Ujihusishaji ya Giles imetuongoza katika utafiti huu. Data kuhusu vibonzo vinavyoleta dhana ya Ugatuzi vimekusanywa kwa njia ya uchanganuzi wa yaliyomo ambapo nakala 50 za magazeti ya Taifa Leo ya mwaka 2010-2014 zilihusishwa . Mikakati mbalimbali ya kipragmatiki kama vile , matumizi ya jazanda, kinaya, chuku, sitiari, yote yaliweza kubainishwa. Aidha utafiti huu umedhihirisha kuwa matumizi ya kinaya na jazanda katika vibonzo juu ya Ugatuzi ndiyo iko katika kiwango cha juu zaidi kwa asilimia 64% na mengine kuchukua yaliyosalia.

# YALIYOMO

IKIRARI ........ ii

SHUKRANI ........ iii

TABARUKU ........ iv

IKISIRI ........ v

YALIYOMO ........ vi

SURA YA KWANZA ........ 1

1.1 Usuli wa Mada ........ 1

1.2 Tatizo la Utafiti ........ 2

1.3 Malengo ya Utafiti ........ 2

1.4 Nadharia tete ........ 2

1.5 Sababu za kuchagua mada ........ 3

1.6 Upeo na Mipaka ........ 4

1.7 .1 Misingi ya nadharia ........ 4

Mawazo makuu ya Nadharia ya Utambulisho ........ 4

1.7.2 Dhana ya Utambulisho ........ 5

1.8.1 Mawasiliano finyu ........ 9

1.9 Yaliyoandikwa kuhusu Mada ........ 11

1.10.1 Mbinu za uteuzi wa sampuli ........ 13

1.10.2 Ukusanyaji wa data ........ 14

1.10.3 Ufafanuzi na Uchanganuzi wa Data ........ 14

SURA YA PILI ........ 16

2.0 DHANA YA VIBONZO ........ 16

2.1 Maana ya Vibonzo ........ 16

2. 2 Historia na Maendeleo ya Uchoraji Vibonzo ........ 17

2.2.1 Vibonzo Afrika Mashariki ........ 19

2.2.2 Vibonzo nchini Kenya ........ 20

2.2.3 Vibonzo Asilia nchini Kenya ........ 21
2.3 Aina za vibonzo ........ 23
2.4 Mitindo mbalimbali katika uchoraji vibonzo ........ 25
2.4.1 Matumizi ya lugha katika uchoraji wa vibonzo ........ 25
2.6 Sababu za uchoraji vibonzo katika gazeti ........ 37
SURA YA TATU ........ 41
3.0 MAUDHUI KATIKA VIBONZO KWENYE GAZETI LA TAIFA LEO ........ 41
3.1 Jedwali 1: Uainishaji ya Maudhui ........ 41
3.2 Matokeo na Maelezo ........ 43
SURA YA NNE ........ 69
4.0 MITINDO YA LUGHA ZILIZOTUMIKA KATIKA VIBONZO VYA TAIFA LEO ........ 69
4.1 Lugha kama chombo cha Mawasiliano ........ 69
4.2 Lugha kama Kitambulisho ........ 70
4.2.1 Jedwali 2; Mitindo ya lugha ........ 71
4.2.2 Lugha ya kitamathali kama mtindo ........ 72
SURA YA TANO ........ 88
5.0 MUHTASARI, MAPENDEKEZO, NA HITIMISHO ........ 88
5.1 Muhtasari ........ 88
5.2 Changamoto za Utafiti. ........ 89
5.3 Mapendekezo ........ 89
5.4 Hitimisho ........ 90
5.5 Baadhi ya Istilahi zilizotumika ........ 91
MAREJELEO ........ 92
VIAMBATISHO ........ vii

# SURA YA KWANZA

## 1.1 Usuli wa Mada

Utafiti huu unachunguza jinsi swala la ugatuzi linavyoshughulikiwa katika gazeti la *Taifa Leo* chapisho mojawapo la shirika la magazeti 'Nation Media Group Limited' nchini Kenya.
Kulingana na Transparency International Kenya (2014), *ugatuzi* ni hali ya kukabidhi mamlaka kwa watu, kazi, haki zao na wajibu wao na vilivile kuhamisha mamlaka hayo hadi mashinani. Dhana ya Ugatuzi ni wazo jipya nchi Kenya na katika nchi nyingi za bara la Afrika, ni wazo lililowapa wakenya fursa ya kuwachagua watu watakaowawakilisha mashinani kwa mara ya kwanza mnamo mwaka wa 2013 wakenya walipotangaza kuwa na katiba mpya inayobeba dhana ya ugatuzi. Mawazo mapya kama vile kuwa na seneta, gavana, wasimamizi kutoka kwenye kaunti yao na mengine yalisinduliwa.

Ugatuzi si jambo geni katika nchi za nga'mbo, hivyo basi dhana hii inasifika sana katika nchi kama vile Amerika, Nijeria na Msumbuji. Kwao ugatuzi ni dhana inayowawezesha kushiriki katika ugawavu wa mamlaka, madaraka na zamu kwa wananchi. Watafiti wengi wamefanyia utafiti vibonzo bila kushughulikia dhana ya ugatuzi kwa kujikita katika mitindo na maudhui yanavyosawiriwa kwenye vibonzo hivyo, hivyo basi hii inatupa upenyu wa kushughulikia swala hili.

Kutokana na katiba ya Kenya 'Sura ya kumi na moja ya Katiba inazungumzia ugatuzi dhana ya Ugatuzi imeweza kuangaziwa kwa undani hivi kwamba lengo lake likipewa kipawa mbele kuwa, imewawezesha wakenya kuzidi kushiriki na kuwapa nafasi ya kuweza kuamua jinsi ambavyo mambo yanavyotekelezwa nchini. Kutokana na haya waandishi katika gazeti la *Taifa Leo* waliweza kubuni vibonzo ambavyo vinaweza kufanikisha mawasiliano kwa njia ya kipekee kwa kutumia chuku ,jazanda na kwa kuwadhihaki viongozi wetu.

Utafiti huu unaongozwa na nadharia ya Mawasiliano ya kiutambulisho ya Giles (1972 & 1982). Nadharia hii inarejelea dhana ya utambulisho kama kigezo maalum kinachotumiwa kumtambulisha mtu, kundi la watu, jamii au taifa fulani na huwa na vibainishi muhimu navyo ni; lugha, mahali, uchumi, utamaduni, siasa, mavazi, chakula. Haya yote hutumiwa kuukamilisha utambulisho. Nadharia hii inaafiki utafiti huu kwa sababu unashughulikia jinsi

ambavyo mawasiliano huweza kupitishwa kwa kutumia vibonzo ni kwamba lugha lazima ikuwepo na mahali inamotumiwa na hapa tujibana katika gazeti la *Taifa Leo* ili kithibitisha hayo.Ingutia (2012), aliweza kuangalia matumizi ya vibonzo katika gazeti la 'The Standard' na 'Daily Nation' kuangazia swala la uchaguzi wa 2007jinsi vibonzo hivyo viliweza kuzua kura kwa wagombeaji wao.

## 1.2 Tatizo la Utafiti

Utafiti huu unachunguza vibonzo katika gazeti la *Taifa Leo* ili kutambulisha na kuchanganua mbinu za kimtindo na kimuundo zinazotumiwa na wachoraji vibonzo katika kuangazia swala la ugatuzi nchini Kenya. Utafiti unaongozwa na nadharia ya Utambulisho/ Ujihusishaji. Vibonzo hutumiwa kuangazia maswala mengi ya kijamii yakiwemo elimu, siasa, ukabila, uchumi, mavazi, ufisadi na kadhalika. Hata hivyo utafiti huu utajikita katika kuchunguza jinsi ambavyo mitindo na maudhui yanavyotumika katika vibonzo vinavyosawiri dhana ya ugatuzi. Naye, David (1995), aliangalia vibonzo kwenye aliangazia jamii ya Uingereza na siasa zao. Kwake vibonzo hutumiwa kuchochea wanasiasa pamoja na uchumi wa kijamii. Tofauti na tafiti hizo, utafiti huu umehakiki maudhui, mbinu za lugha pamoja na mitindo katikavibonzo kwenenye gazeti la *Taifa Leo*. Hili ndilo pengo linalozibwa katika utafiti huu. Kuna haja ya kushughulikia uchanganuzi wa kifani kwa kina katika gazeti la *Taifa Leo* kwani gazeti hili limeandikwa kwa lugha ya Kiswahili linalofahamika kwa wananchi wote kwa kuwa ndiyo lugha ya taifa.

## 1.3 Malengo ya Utafiti

Utafiti huu unaongozwa na malengo yafuatayo:

a) Kuchunguza maudhui yanayotawala katika vibonzo vinavyohusu dhana ya ugatuzi kwenye gazeti la *Taifa Leo*.

b) Kubainisha mbinu za lugha zinazojitokeza kwenye vibonzo hivyo.

c) Kutambulisha mitindo ya lugha inayopendelewa katika vibonzo hivyo.

## 1.4 Nadharia tete

Utafiti huu unaongozwa na nadharia tete zifuatazo:

a) Maudhui mengi katika vibonzo vinavyohusu ugatuzi yamejikita katika ufisadi na yanaonyesha kufaulu kwa ugatuzi nchini Kenya.
b) Lugha ya tamathali na ukiushi ndizo mbinu za lugha zinazotumika sana katika vibonzo vinavyosawiri ugatuzi.
c) Kuwa Sheng' ndio mtindo wa lugha unaopendelewa katika vibonzo hivyo.

### 1.5 Sababu za kuchagua mada

Kwa mujibu wa Iribe na Mukhwana (2011), Kiswahili ni lugha sambazi. Hadi sasa, nchi ambazo zinaitambua lugha ya Kiswahili katika kiwango cha lugha ya kimataifa zimeongezeka.Vilevile, lugha hii inaendelea kupewa umuhimu katika vyuo vikuu ulimwenguni na katika taasisi za elimu. Kwa hivyo kuna umuhimu lugha yake kuendelezwa sio kutoka kwa vitabu pekee bali hata kwa magazeti kama vile gazeti la *Taifa Leo*, linalotufaa katika utafiti huu hasa kwa kuwa limeandikwa kwa lugha ya taifa ambayo ni Kiswahili. Kwa hivyo, utafiti huu unatoa mchango katika maendeleo ya lugha ya Kiswahili. Fani ni kiungo muhimu sana katika kufumbata ujumbe katika kazi ya kifasihi maadamu hujihusisha na umbo nzima ya kazi ya fasihi na vile vile maudhui na fani hutegemeana na kukamilishana. Tafiti kuhusu vibonzo vinavyohusu ugatuzi katika gazeti la *Taifa Leo* ni chache mno, swala la maudhui na mbinu ya lugha haijashughulikiwa vilivyo hasa vinavyosawiri vibonzo kwenye gazeti la *Taifa Leo* ndiyo maana mtafiti anaweza kuyatafitia kwa kina.

Uchanganuzi wa mbinu za lugha katika vibonzo vinavyosawiri ugatuzi unachangia katika usomi wangu wa fasihi. Matokeo ya utafiti huu yanasaidia watafiti katika nyanja mbali mbali kwa kuwa wazo wanalopata kutokana na utafiti huu na baadaye wanaweza kupata mtazamo tofauti kuhusu uchanganuzi wa vibonzo vinavyohusu ugatuzi katika gazeti la *Taifa Leo*. Aidha taaluma ya isimu haitakosa kufaidi utafiti huu kwani maelezo ya mikakati katika vibonzo ambavyo hutumia lugha ya Kiswahili vitaweza kushughulikiwa.

Utafiti huu unaongozwa na nadharia ya Mawasiliano ya Utambulisho. (Communication Accomodation theory ) ya Giles,.H (1982). Nadharia hii inarejelea vibainishi vya jamii ambavyo huzingatiwa wakati wa mazungumzo kama vile sauti, ishara, muktadha, na vilevile huangalia maingiliano ya ishara na maandishi pamoja na vibainishi vyake. Aidha, lugha ya Kiswahili ni lugha ya taifa na rasmi katika nchi ya Kenya, hivyo basi hueleweka na kutumika na watu wengi walio katika pembe zote za nchi, kwa hivyo watu wengi wataweza kuusoma

kazi hii na kuwanufaa. Mawasiliano katika Magazeti hujumuisha maandishi, picha pamoja na michoro mbalimbali ndiyo maana mtafiti kutaka kufanya utafiti wake. Faida ya mawasiliano ya magazeti ni kuwa: ujumbe unaweza kudurusiwa mara kadhaa kabla ya kuusambaza na kuhifadhiwa.Vilevile ujumbe hubaki kuwa ule ule na huwa na wazo nyeti na changamano aidha yaweza kuthibitiwa, kufasiliwa, na kubainisha mawasiliano.

## 1.6 Upeo na Mipaka

Utafiti huu unahusu uchanganuzi wa vibonzo vinavyohusu ugatuzi nchini Kenya kwenye gazeti la *Taifa Leo*. Gazeti hili limeteuliwa kwa kuwa ndilo gazeti la pekee la kitaifa linalochapishwa katika lugha ya Kiswahili nchini Kenya. Kiswahili ni Lugha ya Taifa nchini Kenya, hivyo basi ni lugha yenye utambulisho mkubwa. Uchanganuzi unafanyiwa kutoka kwa vibonzo vilivyo katika gazeti la *Taifa Leo* ambavyo vinahusu ugatuzi. Vibonzo vilivyo chapishwa katika gazeti la *Taifa Leo* kuhusu ugatuzi vitachanganuliwa. Jumla ya nakala hamsini (50) za matoleo ya gazeti la *Taifa Leo* za baina ya mwaka wa 2010 na 2014 zimetumiwa katika uchanganuzi huu.. Hii ni kwa kuwa katiba mpya ya Kenya ilizinduliwa mwaka huo wa 2010. Katiba hiyo ilitumika katika uchaguzi wa mnamo mwaka 2013. Utafiti huu ulianza mnamo Januari 2015; kwa sababu hiyo, utafiti ulihusu machapisho ya tangu kuzinduliwa kwa katiba mpya hadi wakati wa mwanzo wa utafiti. Wakenya waliweza kuwa na serikali ya ugatuzi kwa mara ya kwanza nchini Kenya kuanzia mwaka wa 2013 na hivyo kuwa na maseneta, magavana na wajumbe wa kaunti.Awali, wawakilishi wote walikuwa wa Serikali Kuu.

## 1.7 .1 Misingi ya nadharia

Katika utafiti huu tunaongozwa na nadharia ya Utambulisho /Ujihusishaji ya Giles, H. (1982) kama nadharia kuu.

**Mawazo makuu ya Nadharia ya Utambulisho**

**a)** Huhusika na mahusiano kati ya lugha, muktadha na utambulisho. Giles na wenzake (2005)

b) Nadharia hii huangazia kuwa watu wanapoingiliana wanabadilishana usemi, sauti na hata ishara ili kujihusisha na wengine. Turner na Richard (2010)

c) Hutalii sababu ambazo huwafanya watu kusisitiza kupunguza tofauti kati yao wakati wa mazungumzo.

d) Huangazia sifa za kibinafsi na za makundi ambazo husababisha ujihusishaji na pia huchunguza namna mamlaka, miktadha ya kimaikro na kimakro huadhiri tabia za mawasiliano.

e) Huchukulia kuwa watu huingiza tamaduni na tajriba katika maingiliano kupitia kwa mazungumzo na tabia. Kwa hivyo usemaji na tabia za kufanana hutawala katika mazungumzo.

f) Husadiki kuwa ujihusishaji huathiriwa na jinsi watu huchukulia na kuthamini yale ambayo huendelea wakati wa mazungumzo; kumaanisha namna watu hutafsiri na kuhukumu jumbe katika mazungumzo

### 1.7.2 Dhana ya Utambulisho

Dhana ya utambulisho ni pana mno kwa sababu inafumbata mambo mengi ndani yake. Utambulisho ni jumla ya vigezo maalum vinavyotumiwa kumtambulisha mtu, kundi la watu, jamii au taifa fulani.Vigezo hivi hubainisha kuwa kundi fulani ni tofauti na lingine, jamii moja ni tofauti na nyingine, mtu mmoja ni tofauti na mwingine au taifa moja kuwa tofauti na lingine. Kihore na wenzake (2009), wanasema vigezo ambavyo hubainisha utambulisho wa mtu au jamii vinaitwa vibainishi navyo ni; lugha, utamaduni, historia ya jamii, siasa, uchumi, dini, mavazi na kadhalika.

Nadharia ya Utambulisho iliasisiwa na Howard Giles (1982) .Nadharia hii ya Utambulisho imeendelezwa kutoka kwa Nadharia ya Mawasiliano ya Usemi (Speech Communication Theory) ya Leech (1976). Giles na wenzake (2005), wanasema kuwa nadharia ya mawasiliano ya Usemi ilinuia kueleza hali yanayosababisha mabadiliko katika usemaji kwenye maingiliano ya watu na matokeo ya ubadilishaji huo.Nadharia hii imepanuka kwani haishughulikii namna ya unenaji pekee, bali pia maingiliano mengine ambayo si ya unenaji kama ishara na maandishi.Nadharia hii itatufaa katika utafiti wetu kwani tunachunguza mawasiliano katika jamii kwa njia ya vibonzo.

Utafiti unafumbata mawazo makuu kuwa:

a) Watu wanapoingiliana wanabadilishana usemi, sauti, na hata ishara ili kujihusisha na wengine,

b) Nadharia hii pia huhusika na mahusiano kati ya lugha, muktadha na utambulisho.

Kuna aina mbili za Ujihusishaji; Ujihusishaji wa Makutano na Ujihusishaji wa mwachano Convergence & Divergence)

Wardhaugh (2010) anaeleza kuwa, nadharia ya Utambulisho ya makutano na mwachano iliasisiwa na Giles mwaka wa (1982). Makutano ni namna ambavyo watu hubadili usemi, ishara, na sauti ili kujumuisha washiriki katika mawasiliano.Watu hawa hufanya hivi ili kupunguza tofauti baina yao na kudhihirisha ujihusishaji wao, Giles na Smith (1975). Watu wanaweza kuwa na makutano kupitia njia mbalimbali kama vile: matumizi ya lugha, matamshi, sauti, tabia zisizo za usemi na kadhalika. Ikumbukwe kuwa sio lazima wajihusishe katika mambo haya yote kwa wakati moja.

Hata hivyo , watu wanaweza kuwa na makutano katika kiwango kimoja na kuwa na mwachano katika viwango vingine, Giles na Coupland (1991). Mtu binafsi anaweza kujitolea kujinyima kitu fulani ili naye afaidike kwa kupata ujihusishaji kati yake na wale anaowasiliana nao. Mambo kadhaa ambayo yanaweza kusababisha kuleta makutano ni pamoja na: Utamaduni unaofanana, matumizi ya lugha yanayooana, maingiliano tarajiwa, hadhi, historia, kaida , mamlaka na matamanio ya kibinafsi. Turner na Richard (2010). John-Weiner, (1998) aliyenukuliwa na Wardhaugh anatumia nadharia ya Utambulisho kuelezea namna mbali mbali za uteuzi wa lugha. Anaeleza namna jamiilugha moja inaweza kuamua kutumia lugha kujihusisha na jamii lugha nyingine (makutano ) ama ikatumia lugha kujitenga na jamiilugha nyingine (mwachano).

Kihore na wenzake (2009), wanayaunga mkono maoni haya ya Wardhaugh pale wanaposema kuwa, jamiilugha mbili zinapokutana na kuacha kutumia lugha yao na kuanza kutumia lugha ya jamiilugha nyingine, hapa ndipo tunasema kuwa kuna mkutano kwa jamiilugha mbil. Hii ni kwa sababu jamii lugha hizi mbili huendelea kutumia hii moja inayodumishwa na kutumiwa kwa utambulisho wa jamiilugha hiyo pana.Jamiilugha hizi zikiwa na nguvu tofauti,

jamiilugha dhaifa hubobewa na ile yenye nguvu zaidi.Hali hii inaonyesha kuwa jamiilugha dhaifu haithamini lugha yake pamoja na utamaduni wake.

Iwapo makutano haya yanahusisha kikundi cha wanajamii ambao wanaacha kutumia lugha yao kabisa ili wajitambulishe na jamii lugha nyingine, hali hii inaweza kusababisha kufa kwa lugha. Makutano haya yanaweza kuwa yanaelekea juu iwapo mtu anajihusisha na tabia za watu wa tabaka la juu.Vile vile makutano haya yanaweza kuwa yanaelekea chini iwapo mtu anajihusisha na tabia za watu wa tabaka la chini.

Giles na Byrne (1982) ambao wamenukuliwa na Kihore na wenzake (2009), wanaeleza sababu mbalimbali zinazomfanya mzungumzaji wa jamii lugha fulani aamue kutumia lugha ya jamiilugha nyingine kwa utambulisho wake. Kwanza , utambulisho wa jamii kuonekana kuwa haina umuhimu kwa watumiaji wake. Pili, mzungumzaji kutoamini kuwa mahusiano kati ya jamii lugha hizi mbili yanaweza kuwa na manufaa kwa jamiilugha yake. Tatu, mzungumziwa kuiona jamiilugha yake ni jamii dhaifu isiyokuwa na maendeleo kwa wanajamii wake. Nne, mzungumzaji kuiona jamiilugha yake kuwa haina thamani kwa lolote. Tano, mzungumzaji kujitambulisha kwa jamiilugha yake kwa masuala ya ndani tu, lakini kwa masuala ya maendeleo, elimu na uchumi hujitambulisha kwa jamiilugha nyingine yenye nguvu kwa lengo la kunufaika kijamii na kiuchumi.

Kihore na wenzake wanaendelea kusema kuwa nadharia ya makutano na mwachano inajaribu kupima mshikamano walionao wanajamii lugha kuhusu utamaduni wao na lugha yaokama mbinu ya kupima nguvu ya utambulisho wa jamiilugha. Nadharia hii inasisitiza kuwa ni kazi ya wanajamiilugha wenyewe kuhamasika na kukuzalugha yao na kuitumiaili iweze kuelezea amali za jamiilugha, mielekeo yao na makundi yao na jinsi ambavyo lugha yao ni tofauti na lugha nyingine. Makutano huboresha mawasiliano kwani hupunguza mashaka, dukuduku kati ya watu na kufanikisha maelewano.

John-Weiner (1998) aliyenukuliwa na Wardhaugh anatumia nadharia ya Utambulisho kuelezea namna mbalimbali za uteuzi wa lugha. Anaeleza namna jamiilugha moja inaweza kuamua kutumia lugha kujihusisha na jamiiilugha nyingine (makutano) ama ikatumia lugha kujitenga na jamiilugha nyingine (mwachano).

Keller (1989) anaeleza kuwa utambulisho wa mtu umefungamana na mambo mengine kama vile lugha, utamaduni, historia ya jamii, siasa, uchumi, dini, vyakula na kadhalika. Kinachojitokeza hapo juu ni kuwa, kipengele kimoja au viwili havitoshi kubainisha utambulisho wa mtu, jamii au taifa. Kimsingi utambulisho wa mtu umejikita ndani ya utamaduni wa jamiilugha ambako mzungumzaji anayetakiwa kubainisha utambulisho wake ni sehemu yake.

Tabouret Keller anasisitiza dhana ya utambulisho kwa kutaja sifa bainifu tatu za msingi za kuzingatia katika kubainisha mzungumzaji.

a) Kwanza, ni kigezo cha lugha ya mzungumzaji ambapo anauita utambulisho wa nje unaosikika.
b) Pili, ni kigezo cha mahali alikozaliwa mzungumzaji ambako lugha anayotumia ndiyo lugha kuu ya mawasiliano.
c) Tatu, zaidi yote mzungumzaji anapaswa kujiona kuwa sehemu ya jamiilugha na kuwa ataendelea kuitumia lugha yake ili kuidumisha.

Kwa hivyo katika kueleza utambulisho, lugha ya mzungumzaji ni kibainishi muhimu sana.Vibainishi kama uchumi, siasa, utamaduni, historia ya jamii, dini, mavazi na vyakula hutumiwa kuukamilisha utambulisho wa mtu. Hii inamaanisha kuwa ni vigumu kubainisha utambulisho wa mzungumzaji kwa kutumia lugha peke yake bila uchanganuzi wake kwa kuzingatia jamiilugha anayotoka ambako masuala ya utamaduni, mila na desturi ni sehemu muhimu na kiungo cha umoja wa jamiilugha hiyo. Lugha ya mzungumzaji na utambulisho wake ni mambo mawili ambayo hayawezi kutenganishwa, ni kama pande mbili za sarafu moja. Uhusiano wa lugha na utambulisho unaelezwa vizuri kwa kutumia nadharia za Giles , (1982) hapo juu.

Utafiti huu hauwezi kukamilika bila kushughulikia dhana ya mawasiliano, kwa kuwa bila mawasiliano hatuwezi kufanikisha utafiti wetu hivi ni kuwa vibonzo vimetumiwa kuleta dhana ya ugatuzi na kuleta mitindo mbalimbali ya kuweza kuwasilisha mawasiliano.

Dhana ya mawasilano au ishara matamshi imeelezwa kwa njia mbalimbali na wataalam tofauti tofauti. Fluharty na Ross (1966:2), wameeleza kuwa mawasiliano ni uwasilishaji wa ujumbe kutoka kwa mtu mmoja hadi kwa mwinginekwa kutumia ishara au nyenzo fulani. Wanadai kwamba mtuma ujumbe huufumbata ujumbe wake katika nyenzi fulani na kuutuma

kwa mpokeaji. Naye mpokeaji huzifumbata nyenzo hizi ili kuupata ujumbe uliotumwa. Naye Stumai (1990) anadai kuwa dhana ya mawasiliano ni pana na maana yake hutegemea mazingira. Kimsingi, anaeleza, mawasiliano ni usafirishajiwa ujumbe, watu, mizigo,n.k kutoka upande mmoja wa nchi hadi mwingine. Kwa upande mwingine Tuli (1985:7) anaeleza kuwa mawasiliano ni njia zozote zinazowawezesha wanadamu kuathiriana.Isitoshe, katika hali ya ufinyu wake, anaendelea kueleza, mawasiliano ni usafirishaji wa habari au ujumbe kama vile mawazo,maarifa, ujuzin.k miongoni mwa watu.

Nao Bateman na Zeithaml (1993:5) wameeleza kwamba mawasiliano ni upelekaji wa habari na maana kutoka kwa chama kimoja hadi kingine kwa kutumia ishara za kushirikiana.Aghalabu kuna mtuma-ujumbe ambaye huuanzisha mfumo huu kwa kupitisha ujumbe kwa mpokeaji; mtu ambaye ujumbe unamlenga.Mtuma-ujumbe ana habari ambayo angependa kuiwasilisha na anaufuma ujumbe katika ishara kisha mtuma-ujumbe huupitisha au huutuma ujumbe kupitia njia fulani,kama vile maongezi au maandishi.Halafu mpokeaji huufumua ujumbe kama vile kuusoma au kusikiliza kwa makini na kujaribu kufasiri maana ya mtuma-ujumbe. Hatimaye, Davis (1976:22), ameelezea mawasiliano kama upitishaji wa habari na maelewano kutoka kwa mtu mmoja hadi kwa mwingine. Anazidi kufafanua kuwa mawasiliano ni mfumo wa kijamii. Kwa kuzingatia mawazo ya wataalam hawa ni dhahiri kuwa mawasiliano ni usafirishaji wa ujumbe kwa mtuma-ujumbe hadi kwa mpokea –ujumbe kwa kutumia nyenzo fulani.Sperber & Willson (1995), wanasema kuwa mawasiliano kwa muktadha, unaweza kuchukuliwa kama sehemu tu yayanayodhaniwa kuhusu dunia na anayepokea habari.

Nyenzo mbalimbali zinazotumika kuwasilisha ujumbe ni pamoja na picha na michoro, lugha, ngoma, miondoko ya mwili. Lakini katika utafiti wetu tunajifunga katika michoro na lugha kwenye vibonzo ili kuleta dhana la ugatuzi kwenye gazeti la *Taifa Leo*. Hii itatubidi kuangazia aina za mawasiliano zilizopo ambazo mja huweza kushiriki.

### 1.8.1 Mawasiliano finyu

Mawasiliano ya binadamu yanaweza kugawanywa katika aina mbili: mawasiliano finyu na mawasiliano timilifu.

Mawasiliano finyu ni usafirishaji wa habari au ujumbe kama vile mawazo, maarifa, ujuzi n.k miongoni mwa watu kwa njia ya kauli, taarifa, redio au televisheni, magazeti n.k. Hapa uwasilishaji ni wa mkondo mmoja unaoelekea upande mmoja. Mtoa habari ana dhima ya kutoa habari tu na hapokei majibu au habari yoyote kutoka kwa mpokeaji.Naye mpokeaji anapokea tu bila kutoa habari yoyote. Kwa hivyo, aina hii ya mawasiliano ni rahisi na ya haraka kwa mtuma-ujumbe.

Kielelezo cha mawasiliano finyu




Katika utafiti huu tunajifunga kwenye Mawasiliano finyu kwa kuwa kinaweza kutufaa zaidi kwa sababu ujumbe unafasiriwa na msomaji kupitia mbinu zinazotumika kuangazia ugatuzi kupitia hivi vibonzo.

Mawasiliano yanaweza kufanywa kwa kutumia njia mbalimbali ikiwa ni pamoja na maongezi, maandishi, picha/mchoro na ile ya electroniki. Mawasiliano ya picha/michoro na maandishi ndiyo yatakayoshughulikiwa na mtafiti katika utafiti huu.

Mawasiliano kwenye magazeti huwa ni ya kutimiza haja.Wananafsia hudai kuwa kimaumbile sisi ni wanyama wa kijamii, yaani tunawahitaji watu wengine sambamba na vile tunavyohitaji chakula. Iwapo watu watatengwa bila kuwasiliana, watapata matatizo kwani watazongwa na mawazo na hata kukosa uwezo wa kuingiliana kijamii. Tunawasiliana ili kuwaathiri wengine. Ogechi (2002:12). Hivyo basi utumiaji wa vibonzo katika gazeti la *Taifa Leo* huwa ni ya kufanikisha mawasiliano, ijapokuwa wengi huwa wanapuuza kuyazingatia kwa makini jumbe zinazokuwa pale ndani,mara nyingi yaweza kuthibitishwa,kufasiliwa na kubainishwa kwa kutumia data.

Mtafiti anaushahidi kuwa anayozungumzia bila shaka patakuepo na nakala.Vibonzo hutumiwa kuleta swala nyeti/changamano kuonekana rahisi kwa njia ya ucheshi na swala hilo kuonekana silo la tatizo mno; jamii husika hubanwa na janga fulani lakini jinsi ambavyo wabuni wa vibonzo watakavyo iweka ujembe huo itakuwa kwa ustadi.

Mawasiliano katika Magazeti hujumuisha maandishi, picha pamoja na michoro mbalimbali. Faida yamawasiliano ya magazeti ni kuwa: ujumbe unaweza kudurusiwa mara kadhaa kabla ya kuusambaza  na kuhifadhiwa. Vilevile ujumbe hubaki kuwa ule ule hata kama utapitia siku kadha hasa ndiyo maana hata utatufaa katika utafiti huu na hutumia kuwasilisha mawazo nyeti au changamano na pia yaweza kuthibitiwa, kufasiliwa, na kubainisha mawasiliano.

## 1.9 Yaliyoandikwa kuhusu Mada

### Utangulizi

Sehemu hii inatathmini maandishi mbalimbali yanayohusiana na mada ya utafiti. Miongoni mwa maandishi yatakayorejelewa na kutathminiwa ni yale yanayohusiana na dhana ya vibonzo katika gazeti la *Taifa Leo.*

Kirschen (1981), katika kazi yake anasema kuwa, wachora vibonzo hutumia taswira ya sitiari na karagosi kupasha habari za siasa vya karibuni kwa njia ya ucheshi nakuweza kunata hisia.Anaendelea kusema kuwa katuni vinachorwa kwa njia ya kipekee ya kufanya watu kucheka,na kuweza kujisahau na kuweza kuona mambo kwa njia ya mchoraji wao.Anazidisha kusema kuwa vibonzo kazi zao ni kushawishi kuliko kuchukiza. David, (2005) kule Uingereza, ambapo aliangalia vitabu vya mikono ‘Pocket Cartoonist HandBook’ kwa kuangazia swala la siasa bila matamshi ya vibozo alichoshughulikia ni taswira ya vibonzo kwa jamii. Tofauti na vibonzo vyetu ambavyo vinaambatishwa na maneno katika gazeti la *Taifa Leo* ambapo tunachanganua maudhui pamoja na mitindo ili kuweza kufanikisha utafiti huu.

Scrawl, (2005), anasema kuwa vibonzo vya kihariri pia hujulikana kama vibonzo vya siasa na hulenga kuwasilisha jumbe za kisiri au kimafumbo  kwa jamii wanamoishi, yeye aliangazia jamii ya waingereza. Hivyo basi vibonzo hivyo hubeba chuku pamoja na kejeli nyingi ili kunata uozo ulioko katika jamii.Washiriki hutumia majina bandia, misimbo fiche, ishara au mchoro pekee. Mtafiti ataweza kudhibitisha haya kwa utafiti huu.

Naye Angumbi (2011), utafiti wake ulikuwa kwenye magazeti mawili, The Standard na Daily Nation ambapo aliangazia swala la maudhui kwa jumla. Hivyo basi utafiti wake utafaa

katika utafiti wetu maadamu mada yake ina uhusiano na ya utafiti huu japokuwa unatumia gazeti la *Taifa Leo.*

Ingutia (2012), aliandika kuhusu vibonzo katika gazeti la The standard aliangalia jinsi ambavyo vibonzo viliweza kutumika katika uchaguzi wa 2007 jinsi utumiaji wa vibonzo hivyo viliweza kuvutia voti kwa wasimamizi wa vyama tofauti tofauti pamoja na madhara yaliyoletwa na vibonzo hivyo kwa kuzua hisia mbali mbali. Utafiti wetu utaweza kufaidi kutokana na utafiti hiyo ingawaje tumejikita katika gazeti la *Taifa Leo* na tena kujibana zaidi katika dhana ya ugatuzi.

Musamali (2012), anasema kuwa kazi ya wahariri ni finyu kwa kuwa hawarejelei kwa kina zaidi dhana ya kutumia ufasiri wa kipragmatiki katika diskosi mbalimbali katika gazeti la *Taifa leo*. Tofauti na utafiti wetu ambapo tutaweza kuchunguza kwa kina zaidi matumizi ya vibonzo kuhusu suala la ugatuzi katika gazeti la taifa leo ambapo tutaweza kuangaza mikakati mbalimbali kama vile jazanda, kinaya, chuku na kadhalika kuwasilisha mawasiliano ya vibonzo: hakutueleza jinsi ambavyo vibonzo hutumia mbinu za lugha kufanikisha mawasiliano.

Wabuni wa vibonzo mara nyingi huwa wanajulikana na wakati mwingine wasijulikane. Nafasi wanaopewa huwa ni ndogo kwenye gazeti lakini huibua hisia nyingi kwa wale ambao huielewa. Katika nchi ambazo wasanii wa vibonzo wako wengi mara nyingi hao hujitokeza kuonyesha usanii wao kwa wenzao. Katika nchi hizi, wasanii huandaa mashindano ili kuonyesha umaarufu wao. Hali hii huwafanya hawa kutumia ubunifu mkubwa ili kuvutia wasomaji tofauti na nchi yetu ambayo wasanii hawa hawajapewa umaarufu huo. Kama vile tuzo la ‘Sigma Delta Award’ kutoka kwa jumuia ya waandishi, vile vile kuna ‘Thomas Nast Award’ kutoka kwa waandishi wa habari.

Kulingana na ‘Transparency International Kenya (2014)’, Katiba ya Kenya imebeba majukumu yote pamoja na kanuni ‘objects & principles’ ya uongozi na ni chini ya hii uongozi ya Ugatuzi tunapata mabadiliko ya uongozi chini ya sheria ya 2012, ‘Transition - Devolved Government Act, 2012’. Kimsingi vibonzo hutumiwa kama viwakilisho vya sauti za wanajamii na hutumiwa kutoa maoni, mawazo au ujumbe kuhusu maisha kama vile siasa, elimu, uchumi dini, na maswala ibuka katika jamii. Hivi hutumiwa kama njia mwafaka ya

kujieleza na hutumia namna ya kipekee ambapo tunachukilia dhana la ugatuzi kuyafikisha haya.

Heymans & Mwangi (2013), wanasema kuwa ugatuzi katika nchi ya Kenya inawapa jamii fursa ya kuweza kujitimizia matakwa yao bila kuweza kuenda kwenye ofisi ya serikali kuu,'National Government', kuwa inawapa msimamo waliwezekanalo kwa kuongozwa na matukio katika kuamua jambo la kufanya.Wanazidi kusema kuwa dhana ya ugatuzi huleta mpango taratibu ya kuleta maendeleo nchini kwa kuzuia ukandamizaji wa wananchi na pia kuwa na msimamo wa kutegemea mazuri katika kaunti yao.

### 1.10.1 Mbinu za uteuzi wa sampuli

Utafiti huu utahusu uchanganuzi wa vibonzo vinavyosawiri dhana ya ugatuzi nchini Kenya. Kwa mujibu wa Mugenda na Mugenda (1999: 42), Vibonzo kuhusu ugatuzi vilivyochapishwa katika gazeti la *Taifa Leo,* vinatumiwa kama sampuli ya kufanyia utafiti huu. Sampuli hii inateuliwa kidhamirifu kutoka katika nakala za gazeti la *Taifa Leo* za baina ya mwaka wa 2010 na 2014. Kipindi hiki cha miaka minne kinaweza kuzua kila mwaka vibonzo 365 kwa jumla 1,460 magazeti yaliweza kusajiliwa na gazeti hamsini zilipatikana kuwa na dhana ya ugatuzi , kwa sababu vibonzo vinavyoashiria dhana ya ugatuzi zilianza kuchapishwa baada ya katiba mpya kutangazwa na bila shaka huwa hazichapishwi kila siku bali huwa haiwezi kutabirika wakati gani hasa ingawaje hata kabla ya katiba mpya kulikuwa na michoro hizo za vibonzo lakini kwa kuangazia mada tofautitofauti. Kipindi kinacho teuliwa kinatupa idadi tosha ya nakala za magazeti ya *Taifa Leo* yatakayotumiwa kupata sampuli yetu. Jumla ya nakala zote hamsini (50) zenye dhana ya ugatuzi zinazopatikana kutoka katika gazeti la *Taifa Leo* baina ya mwaka 2010 na 2014 zimetumiwa katika uchanganuzi wetu. Uteuzi wa sampuli hii umekuwa wakidhamirifu ili kuondoa mapendeleo yoyote. Kulingana na mtaalamu Trochin (2006), katika usampulishaji wa aina hii ya kidhamirifu huwa tunasampulisha tukiwa na dhamira fulani akilini.

### 1.10.2 Ukusanyaji wa data

Kwanza, uchanganuzi wa yaliyomo umefanywa ili kutambua kuwepo kwa vibonzo katika gazeti la *Taifa Leo* juu ya ugatuzi. Kila nakala ya gazeti la *Taifa Leo* inayohusishwa katika utafiti umechanganuliwa ili kubaini aina ya maudhui na mbinu za lugha zinazojitokeza katika kila kibonzo. Hali kama hii ndiyo huenda ikawa hutatua kueleweka kwa ujumbe ambao huwa umedhamiriwa kufikia hadhira. Sio wengi hutilia maanani vibonzo hivyo wala kusoma ujumbe ulioko pale. Haya ndiyo sababu mtafiti kutaka kuonyesha kuwa vibonzo vile huwa na maswala yanayosawiri jamii na huwa nyeti lakini huangaziwa kwa njia ya ucheshi na kinaya mwingi. Data hii imelezwa na tathmini kutolewa.

### 1.10.3 Ufafanuzi na Uchanganuzi wa Data

Utafiti huu unazingatia muundo mseto wa utafiti ambapo muundo wa kitathmini na kitakwimu unajumuisha maelezo ya fasiri mbalimbali ya msomaji kuhusu vibonzo vilivyobeba dhana ya ugatuzi. Strauss & Corbin (1990) wanatetea hoja kuwa utafiti wa kitathmini, humsaidia mtafiti kuelewa namna matukio mbalimbali yanavyoathiriwa na hali halisi ya maisha. Kwa upande wao Jonhson & Onwuebuzie (2002), wanatoa hoja kuwa utafiti wa kitathmini ni bora kwa kuwa mtafiti anaweza kutumia tukio fulani kudhibitisha wazi wazi tukio lingine muhimu kwa wasomaji kupitia maelezo. Muundo wa kitakwimu utatumiwa kuelewa tukio ambalo halijulikani.

Aidha, unasaidia katika upatikanaji wa ufahamu mpya ulio tofauti na hali inayojulikana, Strauss & Corbin (1990). Muundo huu pia unawezesha utafiti huu kubaini kiwango cha utokeaji ambacho kinaweza tupa idadi kwa asilimia wa mikakati mbalimbali katika vibonzo vinavyohusu ugatuzi katika *Taifa Leo*. Matumizi ya vipimo vya asilimia vinatumika kudhihirisha utukiaji. Tafiti zilizojishughulisha na uchanganuzi wa matini (eggins 2004; 192) Fairclough (2004) zinatumia uchanganuzi wa kitakwimu kutimiza uchanganuzi wa kitathmini unatumiwa kama mbinu ya kueleza matokeo ya kitathmini, huku uchanganuzi wa kitakwimu ukitumiwa kusisitiza vipimo pamoja na vipengele vinavyokuwa vinatafitiwa maadamu muundo mseto wa kitathmini na kitakwimu ni muhimu sana utafiti wa kitathimini hukusanya data ambayo haiko katika hali ya takwimu. Data ya aina hii ya kitathmini huwa ni ya maelezo na kwa hivyo huwa na changamoto katika uchanganuzi wake ikilinganishwa na ile ya

kitakwimu. Kwa upande mwingine, utafiti wa kijaribati hukusanya data katika hali ya takwimu. Data kama hiyo huweza kupangwa katika kategoria na kuorodheshwa katika viwango mbalimbali. Aidha data hiyo unawasilishwa katika majedwali ambayo hufanikisha kueleweka na vile vile kurahisisha uchanganuzi wake.

**Hitimisho**

Utafiti huu unaweza kuwa msingi mzuri kwa utafiti mpana kwa nyanja nyingine kama vile fasihi, semantiki, sosholojia n.k. Aidha sura hii imeangazia nadharia ya Mawasilano ya Utambulisho ya Giles (1982) yanayozumgumzia namna ambavyo lugha inaweza kuwa kitambulisho cha mtu kwa kutumia vibonzo. Watafiti waweza kufaidika kutokana na fasiri mbalimbali za jumbe zinazoweza kujitokeza kwa kupitia vibonzo na hata mitindo inayotumika huweza kuwafaidi katika kazi zao

# SURA YA PILI

## 2.0 DHANA YA VIBONZO

### 2.1 Maana ya Vibonzo

Etimolojia ya neno katuni ni lugha ya Kiitaliano lenye maana 'cartoon' kumaanisha bodi ya muriali. Hili lilitoka kwa kuambatanisha maneno carton wa lugha ya kiitaliano kwa kazi iliyokamilika ya picha iliyoko kwenye bodi.

Kwa mujibu wa Ingutia (2012), na Mulando (2014), kibonzo ni picha inayochorwa, aghalabu kwenye magazeti, vitabu, na ambayo hueleza wazo kwa namna ya kuchekesha ambayo huleta mwangaza katika jamii, hivi kuwa yanayosawiriwa huwa ni mambo yanayohusu jamii kwa wakati huo. Wanazidi kusema kuwa vibonzo hutumiwa kunata msomaji ili kuzua hisia tofauti tofauti. Msingi mkuu ya vibonzo vya kisiasa ni kufanya wanajamii na wanasiasa kuwa kitu kimoja. Japokuwa kazi yake ni kurahisisha uelewa wa shida zinazowakumba au jambo tu linalozuka kwa njia ya ucheshi na kiweze kuonekana kuwa mwepesi kwa njia tofauti tofauti.
Feldman (2005), anaufafanuzi wake kwa kusema kuwa, vibonzo vya kuhariri ni picha inayowakilisha jamii, kwa kutumia, jazanda, chuku,sitiari, ili kuleta dhana ya siasa inayolenga mtu, watu, kikundi fulani, au hata nchi kwa jumla. Fox na Hoffman (2011), wanakubaliana na Feldman kwa kusema kuwa, vibonzo hutoa maelezo ambayo maandishi pekee kwenye gazeti hayawezi kuleta kama vile, tashbihi, tashtiti, sitiari, kinaya kejeli .n.k. Lengo kuu likiwa ni kuchochea wasomaji kwa njia tofauti licha ya vibonzo hivyo kuwepo magazetini.

Naye Scrawl (2005), anasema kuwa vibonzo vya kuhariri pia hujulikana kama vibonzo vya siasa, kwake vibonzo ni mchoro uliochorwa kwa ufundi kuwasilisha jumbe za kisiri au mafumbo kwa jamii wanamoishi. Aliangazia swala hili kwa kujikita katika jamii ya Waingereza. Zaidi ya hayo aliendelea kueleza kuwa vibonzo hubeba chuku pamoja na kejeli nyingi ili kunata uozo ulioko katika jamii na washiriki hutumia majina bandia ,msimbo fiche, ishara au mchoro pekee kudhihirisha hayo.

David (1995), anasema kuwa katuni ni picha za tashtiti, aliweza kuangalia vibonzo na kufafanua kama skechi kwenye vitabu, na huwa vinaleta taswira ya jamii. Alichunguza jamii ya Uingereza katika kipindi cha malkia kutawala. Wakati huu alishughulikia namna ambavyo

siasa ya malkia ilivyoendeshwa. Kutokana na fafanuzi hizi, tunaweza kujumlisha mawazo haya yote kwa kusema kuwa: Kibonzo ni picha inayochorwa, aghalabu kwenye magazeti, vitabu, na majarida na ambayo hueleza wazo kwa namna ya kuchekesha na hiyo huwa ya kuleta mwangaza katika jamii. Labda kuwa yanayosawiriwa huwa ni mambo yanayohusu jamii kwa wakati huo.

Kwa kawaida, watu wengi huwa hawasomi gazeti la *Taifa Leo*, ingawa huwa limeandikwa kwa lugha ya kitaifa, Kiswahili ambayo kila mmoja huweza kuifahamu.Vibonzo vilivyoko pale gazetini vilevile huwa hayatiliwi maanani kamwe na watu wengi japokuwa huangazia suala linalowakumba wanajamii.Tunasisitiza kuwa kama wasomi wa lugha na jamii, vibonzo vina mahali pao katika kumulika jamii na kuikosoa pale inapoelekea kupotoka.

## 2. 2 Historia na Maendeleo ya Uchoraji Vibonzo

Sanaa ya uchoraji ina historia ndefu. Uchoraji wake ni sanaa ambayo imeenziwa kwa miaka mingi tangu enzi za kabla ya ukoloni, na bado inaendelea kupata umaarufu; kihistoria, vibonzo ni michoro inayopatikana katika magazeti, vitabu, majarida na kadhalika.

Vibonzo vimekuwa tangu enzi za zamani hasa katika nchi za ugaibuni. Dhana hii ni pana kwa kuwa chimbuko lake hasa ni kipindi cha mamlaka ya Malkia aliyekuwa akiongoza Uingereza wakati huo.Kazi za tashtiti za picha za William Hogarth 1763, yakisiwa kuwa kazi za mwanzo za vibonzo katika magazeti. Aliweza kuangazia suala la uozo katika jamii. jamii alimokuwa kwa kutumia vibonzo vya kusawiri siasa.Aliweza kulenga ufisadi ulioko katika karne ya kumi na nane (18) huku akijijikita kwenye siasa za Uingereza.

Kazi za mwanzo zilizoangazia jamii kwa kutumia vibonzo kwenye gazeti ni pamoja na 'Emblematical Print South Sea scheme' 1720, iliyohusu soko la biashara iliyodorora na iliweza kuitwa 'South Sea Bubble' ambayo Waingereza wengi wiliweza kupoteza pesa zao nyingi sana.
Iwapo vibonzo vilikuwa na umuhimu kama huu enzi hizi, kwa nini usiwe na umuhimu sasa? Maswali kama haya ndiyo yaliwafanya watafiti wawili Abel na Buckley 1977 kuuliza; ikiwa sanaa na fasihi za tamaduni fulani huchunguzwa ili kuelimisha jamii; kwa nini katuni isipewe nafasi kama hiyo? Maswali kama haya ndiyo tunayosisitiza katika tasnifu hii.

Vibonzo mara nyingi hushughulikia masuala ibuka katika jamii kwa wakati huo.Kwa mfano kampeni za uchaguzi, visa vya ufisadi, uchumi, usalama, elimu na kadhalika. Kwa hivyo nyingi hazina uhusiano ya moja kwa moja na wabunifu wao.

Utumiaji wa vibonzo katika magazeti yalianza katika karne ya kumi na nane 18, hasa katika kipindi cha mapinduzi ya Ufaransa chini ya James Gillray na Thomas Rowlandson; walioweza kutumia vibonzo kuwakejeli na kuwadhihaki viongozi hasa George iii, aliyekuwa ameshika hatamu ya uongozi wakati huo na zaidi kuangazia suala la mapinduzi chini ya Napoleon wa Ufaransa.

George Cruikshank aliibuka katika nyanja ya vibonzo baada ya Gillray baina ya mwaka wa 1820-1840. Ubingwa wake ulisifika zaidi alipochora vibonzo vya siasa kumhusu familia ya malikia na wanasiasa, washika hatamu ya uongozi wakati huo, jinsi ufisadi ulivyokithiri katika serikali ya Malkia 1820. Kazi zake zilizosifika sana huo ni uhuishaji wa Uingereza iliyoitwa 'John Bull' iliyokuzwa 1790, pamoja na kazi zingine za kuwakejeli wanasiasa na hii pia iliweza kukejeliwa na James Gillray na Thomas Rowlandson.

Ubunifu wa vibonzo ilizuka kwa kuchapishwa kwa jarida la 'Punch 1841' ilichovumbuliwa na Henry Mayhew na Ebenezer Landells. Gazeti lililosifika kuchapisha vibonzo kila mwezi wakati huo liliitwa 'Monthly Sheet of caricature' lilipigwa chapa 1830 na liliweza kuwadhihaki jamii kwa njia ya ucheshi hasa viongozi.

Neno katuni lilitoka kwa kuambatanisha maneno '*carton'* kwa lugha ya kiitaliano kwa kazi iliyokamilika ya picha iliyoko kwenye bodi na lilichapishwa katika gazeti la 'Punch' na hapo ndipo neno katuni lilianza kusifika sana. Neno hilo ni la Italiano kumanisha bodi ya kuunganishwa. Yaaminika kuwa ndiyo yaliyounda vibonzo vya kuchekesha kutoka wakati huo. Mchoro ya nahodha Pope Urban viii iliwasilisha mchoro ulioko na chuku mwingi kuhusu sifa za wanasiasa wa kipindi hicho. Asili ya vibonzo yaaminika kutoka Meditereniani. Ukuaji wa vibonzo uliweza kuchochewa sana kwa kutojua kusoma kwa jamii katika kipindi hicho na jinsi wakati ulivyozidi kupita na ndivyo watu walivyo zidi kuzitumia kama vile Wajerumani waliweza kufuata mkondo wa wataliano wa kuchora vibonzo na haya yalienea sana katika karne ya kumi na nane, ikawa mbinu mojawapo ya kupitisha ujumbe katika jamii.Haya yote yalifanywa kwa ufundi mwingi wa kuleta ucheshi katika wasomaji bila shaka na kuzua mjadala.

Mwana katuni wa Amerika aliyezaliwa kule Philadelphia na kusifika sana kutokana na kazi yake ya ukatuni ni Benjamin Frankline kazi yake ya 'Join or Die 1754' iliyokuwa ya joka kubwa mno lakini joka lenyewe lilikatwa vipande vipande nia yake lilikuwa ni kuchochea wamerika kuwa kitu kimoja japokuwa walitoka kwenye koloni tofauti tofauti ,kwa hivyo alitaka kuwaunganisha pamoja. Karne ya kumi na tisa ilipofika, vibonzo vya kuharirіwa vilikuwa vitu vya kawaida katika magazeti kule Amerikani.

Wasanii walioweza kuchapisha kazi zao katika gazeti hili waliitwa ndugu wa gazeti hili Charles Dickens ikiwa mmoja wao 'The Punch Brothers' baina ya mwaka wa 1840 kuendelea. Waliojiunga nao ni pamoja na Charles Dickens na hao ndio waliokuwa wawanzilishi wa *Evans Literary Magazine* liitwalo 'Once a week' na ilianzishwa 1859. Karne ya kumi na tisa (19) kilijulikana kama kipindi komavu wa vibonzo katika magazeti, kwa kuwa ndicho kipindi kilichozua wabunifu wengi katika nyanja ya uchoraji wa vibonzo. Mfano unaofahamika sana ni ule wa 'Thomas Nast' jijini New York. Nast alijulikana kuwa na kipawa mbele wenye vibonzo vya kuhariri katika gazeti na pia aliweza kuchora vibonzo mia moja sitini na nane (168) vya kumkejeli kazi za Boss Tweeds aliyekuwa mwana siasa mashuhuri wakati huo huko New York.

Naye Albert anasema kuwa Thomas Nast ndiye aliweza kuzua hisia za watu kwenye vibonzo vyake vya kisiasa katika karne hiyo ya kumi na tisa (19).Wengine wanaosifika kwa kazi zao za vibonzo vya kihariri ni kama vile ya Benjamin Frankline 'Join or Die 1759' iliyobuniwa ili kuleta wananchi wa amerikani pamoja.Nyingine ilikuwa 'The Thinkers Club 1819'. Vibonzo hivi viliweza kutumiwa kutoa ule ukali wa maisha katika jamii na kuleta ucheshi kwa njia ya kipekee .

### 2.2.1 Vibonzo Afrika Mashariki

Marejeleo ya vibonzo vya mwanzo katika tarihi za Afrika Mashariki zilihusu wapiganaji wa vita vya dunia ambalo liliitwa 'Jannie in The Jungle' lilikuwa la Uingereza na lilikuwa na kejeli mwingi kumulika nchi hiyo pamoja na 'The International journal of African Historical Studies1981'. Hivi vibonzo vilienea kote Afrika Mashariki. Gazeti la ucheshi lilikuwa ni *Karonga Kronikal* kilichoanzishwa na wanavita, kazi lake likiwa ni kuleta wanajeshi wa Ujerumani katika njia ya ubunifu mkuu kwa kuwachora na sare zao za kivita walivyokuwa ya

kuogofya sana kulingana na jinsi walivyokuwa tofauti na wale wenye vita kutoka Afrika Mashariki waliochorwa kwa njia ya ucheshi huku wakiwa wanafa kama nzi maadamu hawakuwa na uzoefu wa kivita kwa vyovyote.

Philip Mitchel aliweza kuhariri gazeti la *Kronikal,* baadaye aliweza kufanya kazi katika serikali ya wakoloni nchini Kenya.Hawa wote waliandika kazi zao kwa mtazamo wa 'The Punch" ya Uingereza kama mfano wao kwa kushughulikia vibonzo.

### 2.2.2 Vibonzo nchini Kenya

Katika nchi ya Kenya dhana inayohusu vibonzo ni tukio la kila siku kiasi cha kuwa jambo la kawaida katika magazeti. Magazeti yote nchini yana kurasa maalum zilizopangwa kwa namna sawa zenye habari za vibonzo ndani yao. Kwa njia hii uhariri wa vibonzo unaelekea kutoa mtazamo wa mambo yanayolengwa maishani kwenye gazeti.

Gado ndiye msambazaji wa habari za vibonzo vinavyohusishwa na siasa katika nchi za Afrika Mashariki na kati pia ni mwandishi katika gazeti la Daily Nation.Katika gazeti la Taifa Leo mhariri wa vibonzo anajulikana kama Igah, ambaye aliweza kuchukuwa mahala pa Gado baada ya yeye kufurushwa kazi.

Sobania (2003), anasema kuwa gazeti la kwanza kuandaliwa katika nchi ya Kenya ilikuwa ni 'The Africa Standard ilioanzishwa 1902 na mfanyi biashara aliyejulikana kama A.M. Jevanjee pamoja na mzungu mmoja aliyeitwa W.H. Tiller. Wawili hawa waliweza kuja pamoja na lengo lao likiwa ni kuzungumzia kitu kimoja lililokuwa ni kupata uhuru wao na kuleta waafrika pamoja. Ingawaje nyanja hiyo ilikuwa ikimilikiwa na wazungu, ilipowadia mwaka wa 1963 waafrika walikuwa tayari wamepata njia ya kuwasiliana kwa kupitia gazeti hili la 'The African Standard.'Hata hivyo walipata changamoto si haba kwa kuwa wazungu walikuwa wakiwazuia mjuhudi yao ya kueneza mambo yao hasa shirika zilizokua zikichapisha habari kwa lugha za kiasili kama vile, Kamba, Swahili, na kikuyu. Sobania (2003), anaendelea kusema kuwa nyingi za uchapishaji kwa wakati huo ilikuwa ni kuhamasisha waafrika kuhusu uhuru wao jambo ambalo liliwakasirisha sana wazungu wakoloni.Gazeti hili la wenyeji ilikuja kubadilishwa jina na kuwa 'The east African Standard' badala ya 'The African Standard.' Gazeti hili liliweza kuwa na matawi yake yaliyozungumzia shughuli za waafrika kama vile, 'Baraza', 'Mombasa Times' na 'The Tanganyika Standard'.Kazi yake imetusaidia kwa kuonyesha kuwa jamii walikuwa wakipata

shida kwa kupitia viongozi wao wa hapo awali.Kwa hivyo waliweza kutumia vibonzo kama njia mojawapo wa kuwasiliana.

### 2.2.3 Vibonzo Asilia nchini Kenya

Vibonzo vya kiasili nchini Kenya vilianzishwa na Edward G. Gitau mnamo mwaka wa 1950, aliyekuwa mfanyi kazi katika kampuni ya umeme, alianza kazi ya uchoraji kibahati tu hivi ni kwamba, alikuwa pia mjenzi basi siku moja alitoka juu ya nyumba na kuanguka na kuvunjika mikono hivyo basi hangeweza kuendelea na kazi yake ya ujenzi alilazimika kufanya kazi mbadala ndipo alipogundua kuwa ana talanta ya uchoraji ikawa ndiyo mwanzo wake wa kuanza kuchora vibonzo vilivyoitwa *Juha Kalulu*.

'Juha Kalulu' likiwa ni kiambatisho kutoka kwenye lugha mbili za kiafrika, 'Juha' kuwa Kiswahili kumaanisha mcheshi na 'Kalulu' kuwa Nyanja lizungumziwalo Malawi kumanisha Sungura. Hivyo basi kuleta dhana ya kuwa sungura katika ucheshi wake kwa kupitia ujanja. Nchini Kenya kazi za ucheshi zilizoenea sana ni vile vilivyoko katika gazeti la ***Tazama***. Vibonzo vilivyochorwa wakati huo na Gitau zilipelekwa katika gazeti lingine pia liitwalo ***Baraza*** kilichochapishwa pia kwa lugha ya Kiswahili.Ijapokuwa Gitau alibobea katika magazeti haya mawili, aliweza kuwachorea magazeti za lugha za mama pia. Gazeti la ***Baraz***a lilianzishwa mwaka wa 1939, na kufika kikomo chake pindi tu kabla ya uhuru.

Gitau mwaka wa 1960, aliweza kuhamisha kazi zake katika gazeti la *Taifa*, kilichoanzishwa kama gazeti la wiki, na baadaye kuwa la kila siku. Kulingana na Gitau wachoraji wa vibonzo wa wakati huo alikuwa ni William Ogutu. Katika kipindi hicho alikisiwa kuwa iwapo vibonzi sio vyake basi ni vya Ogutu na bila shaka vilimiliki jina lake la *Juha Kalulu* .Hivyo basi *Juha Kalulu* kilipata umaarufu wake kwenye gazeti kuwa wa kipekee kwa muda mrefu sana kwa kuangazia maswala ya kijamii kwa jumla; bila kujikita kwa pahala maaluum,hadi alipoibuka Terry Hirst katika miaka ya sabini (1970).
Terry Hirst na gazeti la *Joe*, inaaminika kuwa ndiye mwanzilishi wa vibonzo vya kisiasa nchini Kenya. Alifunga miongo wa sabini na kufungua wa themanini kwa kazi ya kila Ijumaa lililoitwa katika gazeti la 'Daily Nation' iliyokuwa na wafuasi wengi. Alikuwa gwiji katika onyesho la kijamii na kuangazia siasa za mashinani wakiwa wameungana na Hillary Ng'weno miongo wa sabini (1970), na kuanzisha gazeti la *Joe* lilichokuw*a* cha kila mwezimhusika mkuu akiwa *Joe* **,**ambako kwa kupitia waliweza kuangazia uozo katika jamii

pamoja na siasa pamoja na viongozi wa nchi.Tofauti na *Juha Kalulu,* ambalo halikushughulikia siasa katika nchi na viongozi wa nchi, *Joe* liliangazia suala la siasa bila uoga na kwa njia ya vibonzo. *Joe* halikuogopa serikali wakati huo ambalo halikutarajia kukashifiwa.Vibonzo vilivyo tangulia vilikuwa na wahusika wa kubuniwa tu, *Joe* lilikuwa kama anayelenga mhusika fulani mpaka iliweza kuonekana kuwa ni jirani wako anayekujua kabisa. Gazeti hili lilikuja kuleta athari kubwa kwa maisha ya wanajamii kwa kuangazia uozo ulioko kwenye serikali. Gazeti la *Joe* lilichapishwa kwa muda wa miaka mitatu pekee kisha kikatokomea. Licha ya hayo kiliweza kuwapa wanakatuni wengi upenyu katika nyanja ya uchoraji wa vibonzo. Gazeti hili lilipoachwa kuchapishwa kiliweza kuleta mwanya katika nyanja hii ya vibonzo. *Joe* kingali kina kumbukumbu katika mtaa wa Nairobi.

Ng'weno baadaye alianzisha *Nairobi Times* gazeti la kila wiki na kuuzia kwa washika dau wa KANU na jina likabadilika kuwa *Kenya Times*; na lilichapishwa kila Juma pili na *The weekly Review*. *Nairobi Times* lilikuwa ndiyo ya wanavibonzo. Gazeti la *Joe* lilipoachwa kuchapishwa ,Hirst hakusikika tena katika uwanja wa vibonzo, baadaye wanavibonzo wengi waliweza kutoka  nchi zanje nakujiunga na wanavibonzo wa Kenya kama vile, Phillip Ndunguru wa Tanzania, James Tumisiime wa Uganda na Frank Odoi wa Ghana watatu hao walisifika kwa kazi zao za uchoraji wa vibonzo katika magazeti mbalimbali.

Ndunguru alijiunga na gazeti la *Kenya Times1983*, na kuanzisha vibonzo vilivyoitwa 'Kazi bure' kilichopendwa sana kwa kuangazia swala la kijamii. 'Kazi bure' maanake kisicho na dhamana wahusika wake walihusishwa na kuleta uozo wa wanasiasa katika jamii. Ndunguru aliaga 1986, akiwa na miaka midogo sana ishirini na nne tu. Naye Tumisiime alijiunga na *Daily Nation,* na licha ya kuchora katuni aliandika pia vichekesho. Vibonzo alivyovichora angali vinatambulika kama lile lililokuwa na mhusika 'Bogi Benda' mwaka wa 1986 alirudi kwao Uganda na kuwa mwana siasa. Frank Odoi alianza kuchora katuni vya kisiasa kwa gazeti la 'Nation' kuanzia mwaka wa 1979. Kama Hirst, Odoi, Tumisiime na Ndunguru wamekuwa wanavibonzo wa Kenya waliokuwa magwiji wakati huo.
Odoi alipokuwa akifanya kazi katika gazeti la 'East Africa Standard', aliibuka mwana kibonzo mwingine Kirui Koskei ambaye alichukuwa nafasi yake aliporejea kwao. Naye Paul' Madd' Kalemba, ndiye mwanzilishi asilia wa vibonzo vya kisiasa. Aliungana na 'Nation' 1986, kama mhariri wa katuni .Kutokana na ucheshi wake aliyoionyesha kwa kupitia kazi zake alipata jina la utani wa 'Maddo'. Kulingana na Agunda John waliangazia maswala yote ya kisiasa pamoja na ya kijamii. Katika Miaka ya 1980, vibonzo vya mwanzo vya kuhariri

viliweza kuchapishwa katika magazeti ya kila siku lakini zilizuiwa kuangazia maswala nyeti za serikali na hawakuruhusiwa pia kuchora chochote kumhusu rais, na washika dau wa kiserikali. 'Madd' anasifika kuwa mwanakatuni wa kwanza kuweza kumchora rais wa wakati huo Daniel Arap Moi. 'Madd'alijiunga na 'Standard' pamoja na mwenyeji wa Tanzania Godfrey 'Gado' Mwampembwa alichukuwa nafasi yake katika 'Nation' na kuendeleza kazi ya uchoraji wa vibonzo ambapo aliweza kusifika na kupata tuni si haba katika kazi hiyo Afrika Mashariki na kati. Kazi zake ziliweza kuchapishwa katika magazeti za nje kama vile, 'New African' kule Uingereza 'Courier International', 'Lemonde' kule Ufaransa; 'Financial Mail' na 'New Nation' zote kule Afrika Kusini.'Washington Times', 'Des Stand' ya Ubelgiji pamoja na 'Japan Times'.

Hivi leo kila shirika la uchapishaji linamiliki wanavibonzo ambao wanalipwa kutokana na hiyo kazi yao.Vibonzo hivyo vina kurasa vyao maalum kwa mfano katika gazeti la *Taifa Leo* linapatikana katika ukarasa wa kumi na moja. 'It's Madd Madd World', kama kitambulisho chake kama mwana katuni katika arena ya kisiasa na maswala mengine yanayokumba wanajamii.

Kwa kuhitimisha, tumegundua kuwa vibonzo vimekuweko tangu miaka ya 1859 na hatutarajii kutoweka. Hii ni kwa sababu matatizo ya wanajamii ambayo hayatatuliwi hujitokeza katika vibonzo. Hapa ndipo tunapata nguvu katika tafiti za vibonzo kwani vinatuwezesha kuingia kwenye akili za binadamuna kutambua maoni na mawazo yao ambayo pengine hayangejulikana katika hali ya kawaida.

### 2.3 Aina za vibonzo

Kutokana na upana wa vibonzo kuna aina tatu; vibonzo vya filamu, vibonzo vya michoro na vya picha (Cambridge International Dictionary of English (1995).

a) Vibonzo vya michoro

Kulingana na Bohl, (1999), anasema kuwa hizi  ni vibonzo vinavyochorwa na wasanii mbalimbali kwa njia ya kuchekesha na hutumiwa kuibua swala nyeti inayokumba wanajamii.Vibonzo hivi huchorwa kwa ubunifu mwingi mno ikiambatishwa na maneno

yanayoweza kuzua hisia mbalimbali kulingana na mtu binafsi. Maneno hayo huwa yana mwigo wa wahusika wanaodhamiriwa kuwa walisema maneno yale. Naye (Obonyo :2004; 109), anamaoni kuwa aina hii ya vibonzo lina jukumu la kuchekesha na kutoa uchuvu ulioko. Anaendelea kusema kuwa vibonzo vya kihistoria hutumika kama kumbukumbu lakini pia kuangazia jamii jinsi wanavyotumia lugha katika mawasiliano na kuendeleza utamaduni.
Katika utafiti huu mtafiti amejifunga katika vibonzo vya kuchorwa katika gazeti la *Taifa Leo* vya kila siku kwa sababu wabunifu wao huangazia masuala ya kijamii kiwakati.

b) Vibonzo vya filamu

Vibonzo hivi pia huitwa vibonzo hai na hutumiwa kama njia mojawapo ya kuburudisha na kutoa uchovu kwa njia ya kipekee, hupatikana katika runinga na video na kadhalika. Vibonzo hivi huwa ni picha tofauti tofauti iliyowekwa pamoja na kuwekewa uhai na huiga vitendo vya binadamu kwa kutumia wahusika mbali mbali ambao huweza kuwa binadamu au wanyama kama vile, paka na panya kama vile filamu ya *The Simpson, Superman, Spiderman, Tom na Jerry, Garfield, Scooby Doo* na kadhalika. Huwa zina vipande vingi tu vilivyoungwa pamoja na huwa na ile kichocheo kikuu mwishoni mwao, Feldman (2005).

c) Vibonzo vya Paneli

Lordan (2006), anasema kuwa aina hii ya vibonzo huwa kwenye paneli moja. Kibonzo hapa huwekwa ili kuweza kutoa hadithi fulani inayosisimua, lakini kwa mtazamo wa yanayofanyika katika jamii kila uchao.Kila mara huwa na kinacho chochea wasomaji wakechini ya paneli hiyo. Kwa mfano *Bogi Benda, Phantom, Spiderman* na kadhalika. Hata vitabu vya aina hii huwa na huwa na uendelezo wa hadithi, kama vile *Tin Tin, Pink panther* n.k. Vibonzo ni mojawapo wa Zeitgeist. Kwa kuvitazama vinaleta dhana ya Zeitgeist wakati vinapo chapishwa. Kwa hivyo vibonzo vya miaka ya hamsini 1950 vinatuelezea jinsi ambavyo dhana ya ukolono ulivyoendelezwa, (Cuccolini, 2002 :66).

### 2.4 Mitindo mbalimbali katika uchoraji vibonzo

Mitindo mbali mbali imeweza kuwapa wachoraji nafasi ya kuchora jinsi watakavyo. Kuna kuchora tu picha bila kuambatisha maneno yoyote na kuna vibonzo vinavyoambatishwa maneno kwenye picha fulani; ili kuwasilisha ujumbe wao. Katika utafiti huu umejikita katika sura zote mbili za vibonzo kwa kuwa njia zote zimetumiwa na mwandishi uwasilisha ujumbe wake.

#### 2.4.1 Matumizi ya lugha katika uchoraji wa vibonzo

Kwa kweli sio watu wengi hutilia maanani vibonzo vilivyoko pale kwenye gazeti la *Taifa Leo*, na iwapo hao huona picha hizo huwa hawadhamiriwi kuwa huweza kuwa na ujumbe nzito.Picha hizo hujitosheleza na kufanikisha mawasiliano.Vibonzo hivi huwa vimeambatishwa na maneno ambazo kwa kawaida huwa ni ishara ambazo zina mpangilio maalum. Ishara hizi zinaunda vipashio vikubwa kama, mofu, maneno, virai, vishazi na sentensi. Vipashio hivi hupangika ili kuleta maana katika mawasiliano. Hivi ni kusema kuwa, maneno kwenye vibonzo vina msimamo wa kiisimu wa Kifonolojia, Kimofolojia, Kisintaksia, na Kisemantiki.

Wachoraji wa vibonzo huwa wanajulikana. Nafasi yao huwa wametengewa japokuwa huwa ni ndogo. Katika *Taifa Leo,* ukarasa kumi na moja huwa imetengewa kuwa vibonzo vya Igah, ambalo si jina lake kamili.Wabunifu hawa huwa huru kuchora vibonzo bila vizuizi vyovyote na hali hii huibua vibonzo ambavyo vina ubunifu mwingi.

Katika nchi ambazo wachoraji wa vibonzo wanatambuliwa, wasanii hao hujitokeza kuonyesha usanii wao wa uchoraji kwa wasanii wengine na hata kijishindia taji kama vile ‘Gado’aliweza kutuniwa ughaibuni licha ya kuwa Mwafrika kutoka Tanzania. Hali hii huwafanya waandishi hawa kutumia ubunifu mkubwa ili kuwavutia wasomaji wa gazeti hilo.Vibonzo vichoravyo huweza kuwa wazi na vingine visiwe wazi. Washiriki pia hutumia majina bandia , misimbo fiche, ishara au alama zenye mitindo ya kipekee.

Uhuru mwingine wa wachoraji wa vibonzo ni kuwa, huwa hawafungwi katika sheria za kiisimu. Uhuru huu ndio huwapa nafasi ya kuonyesha ubunifu wao vilivyo.

Tunaangazia namna wachoraji wanavyotumia lugha kuwasilisha mawasiliano katika gazeti la *Taifa Leo*. Ukiukaji wa matumizi ya sarufi sahihi ya Kiswahili ni pamoja na;

a) Makosa ya tahajia imeweza kutambuliwa. Makosa ya herufi kubwa pale ambapo inapaswa kuwepo lakini iliweza kupuuzwa, huenda ilifanywa kimaksudi au sio.
Katika kazi hii vibonzo vimepangwa kutoka nambari 1-50 na vitaweza kutumika katika kazi yote kulingana na mahitaji ya kazi hii.

Mfano; 1 Vibonzo #9, #50




Tazama kibonzo kilichoko hapo juu, Serikali kuu badala ya Serikali Kuu,k wa hivyo ukiukaji uko pale.




Kibonzo # 50, Hazina ya vijana badala ya Hazina Ya Vijana

b) Kufupisha maneno

Hapa tunaona Akronimu metumika, lengo likiwa ni kuonyesha ubunifu wao na kuvutia wasomaji lengwa.


Mfano: 2   Kibonzo # 10. MCA badala ya Members of County Assembly.




Kibonzo # 15. ATM badala ya Auto Teller Machine na Mpesa- Mobile Pesa




Kibonzo  # 19. R.I.P badala ya Rest In Peace




c) Dhana ya uhuishi pia imeweza kujitokeza katika vibonzo vingine. Tunaona wasanii kuwaweka wafu kuwasiliana wakiwa kaburini licha ya hao kuwa wafu. Marehemu ya kwanza aliaga kabla ya uchaguzi wa 2007 na wa pili punde tu baada ya uchaguzi wa 2007, wakati ambapo palizuka rabsha baada ya kura kupigwa.

d) Kuchanganya msimbo

Maneno ya Kiswahili yameweza kutumika pamoja na ya Kiingereza, kuonyesha uelewa zaidi ya lugha mmoja. Kutokana na tajriba walio nao wasanii hawa.

Mfano:  3 Kibonzo # 1, # 2, #19, # 24, # 47.





Katika kibonzo hiki kimetumia zaidi ya lugha moja. ‘ Mhusika aliyepale kutaka kuandikisha chama chake cha MyDressMyChoice kama chama. ‘Naweza kuandikisha MyDressMyChoice kama? Nimeona iko na wafuasi wengi’. Ni kinaya pia kuwa mhusika ni mwanamume lakini anataka kuanzisha chama cha My  dress My choice.




Kibonzo hiki ni cha mwanafunzi anayefanya mtihani, lakini hana uhakika kama atajibu swali kivipi. ‘Sasa hii nitajibu kwa sheng ama sms’ kushiria namna ambavyo wameathirika na lugha ya pili wanayo ifahamu.



Katika kibonzo hiki kuna mhusika mmoja mkahawani ambaye anatumia maneno ‘HATE SPEECH’ kwenye mtandao.




Kibonzo hiki kinaonyeszha wafu wakiwasiliana wakiwa kaburini.’Restless MPIGA KURA’ Mare Hemu Died 2005’. Yote haya  yanaonyesha kuchanganya ndimi.




Tazama namna vibonzo wanawasiliana. ‘Ghost workers wenzangu, usajili unaoendelea unaweza tupeleka ritaya mapema’ na yule wafu wa pili anasema ‘Ahsante Chairman kwa hiyo habari’.

Msamiati ambao unatumika katika vibonzo unategemea mada. Inabidi wasomaji wajikite katika muktadha ili kuweza kuelewa jumbe kwenye kibonzo

e) Miundo ya Sentensi

Sentensi ni kipashio cha tungo kikubwa kabisa kimiundo chenye maana kamili; (Massamba, 2009). Miundo ya sentensi ambayo tumejadili ni pamoja na sentensi sahili na sentensi ambatani.


Mfano4; Vibonzo #2, # 8, #13, # 40, # 42





Walinda zamu wakiwa wameshika doria wakati ambapo nchi iko katika hali hatari ya kuvamiwa na magaidi waliweza kuwasiliana kwa Kiswahili tena iliyo sanifu. ‘Lazima tuimarishe usalama’, ni sentensi sahili.





‘Mtihani wa leo sio mgumu’ ni sentensi sahili na hii iko wazi wakati ambapo mhadhiri anazungumza na mwanafunzi wake.Ya ziada amebebea picha ya mchoro ya mapenzi, huenda anampangia uroda huyu mwanafunzi





Nitakumaliza ni sentensi sahili vile vile kwa kuwa /Ni/ kuchukuwa nafasi ya kiambishi awali tena inachukua nafasi ya nafsi, kuna kiima na kumaliza kusimamia kiarifu.




Wanavibonzo hutumia vipashio vifupi kwa jumbe zake. Maandishi kwenye vibonzo huwa hamna mipaka ya wazi kati ya maneno, virai, au sentensi ili kubainisha sentensi kamili ambayo ina wazo kamili. Sentensi nyingi katika vibonzo huwa ni visehemu au vipande vya sentensi kamili. Hata hivyo katika vibonzo hivi vya gazeti la *Taifa Leo*, wasanii walitumia vipashio vifupi na pia sentensi sahili kwa wingi kama ifuatavyo;

Mfano5; Vibonzo # 36, # 37




Katika kibonzo hiki tunamwona mwanafunzi aliyehitimu na anatafuta ajira, lakini ni wapi kuna ajira kwenye ofisi wa magaidi na hapo ndipo tunapata kipashio hiki kifupi ‘ Karibu ndani’.




Kutokana na kibonzo hiki, tunashuhudia matokeo ya mgomo ya walimu. Mwanafunzi huyu hawezi kufanya vizuri darasani maadamu hakufunzwa vilivyo, ndiposa anasema ‘ ‘Kama sio mgomo…’ pengine angepita.


f) Sentensi sahili/ Vishazi

Sentensi sahili huwa na muundo wa kiima na kiarifu. Kamusi Sanifu ya Isimu na Lugha (1990). Kwa mfano; Vibonzo # 21, # 42 Vinaonyesha utumiaji wa sentensi sahili kwenye vibonzo hivyo.




Katika kibonzo hiki, tunangamua kuwa mwanafunzi huyu anauzungumzi nafsia anaposema, 'Nikilemewa, nitalaumu mgomo wa walimu'. Sentensi ni sahili kabisa, japokuwa yote yamo kwenye mawazo tu. Naye pia analaumu walimu kugoma kuwa chanzo chake cha kutofaulu mtihani.






Tazama kibonzo kilichoko hapo juu, ni binadamu wanaopewa sura ya wanyama. Mmoja ni nguruwe na mwingine ni fisi. Nguruwe kumvisha fisi tunu ni jambo la kushangaza sana, tena ni tuna zinazokera wananchi. Kuna huyo mama anashangazwa na jinsi mambo yanavyoendelea. Fisi huyo ni kiongozi anaye jivunia kuwa Mkenya. ‘ Najivunia kuwa Mkenya’.

g) Sentensi Ambatani

Massamba (2009), anasema kuwa,hii ni sentensi inayotokana na kuunganishwa kwa sentensi mbili ambazo kila moja inajitegemea kimaana. Katika data yetu ya gazetila Taifa Leo, tulipata mfano huu; Kibonzo # 16





h) Virai

Kirai ni kipashio cha kimiundo chenye zaidi ya neno moja lakini ambacho hakina muundo wa kiima na kiarifu.

Mifano ni kama ifuatayo;


Vibonzo # 23, # 37




'Tunaishi kama ndugu na dada' haya ndiyo maneno yaliyoko kwenye kibonzo hiki. Hakina kiima, bali kiarifu tu.




'Kama sio mgomo', ni sentensi kinachoanza na kitenzi kishirikishi kikamilifu, kwa hivyo hakina kiima vilevile.




'Nitakumaliza' ni sentensi sahili /Ni/ ikisimamia nafsi ya kwanza umoja, /ta/ inachukua wakati ujao, /ku/ kinachukuwa nafasi ya kirejeshi, na /maliza/ kuwa mizizi.

i) Ukiushi

Ukiushi katika lugha hujitokeza katika hali tofauti tofauti kwa vile wasanii huwa hawajafungwa katika sheria za kisarufi. Ukiushi huu hutokea katika viwango mbali mbali kama vile;

Kibonzo # 37




Huu ni ukiushi wa kisintaksia wa sababu ya kuanza sentensi kwa kihusishi /kama/. Kwa kawaida katika sentensi ya Kiswahili mpangilio ni ule wa kiima na kiarifu.

Philips (1996), anasema kuwa jamii ambazo hushiriki katika uchoraji wa vibonzo, hulenga kuwasilisha jumbe za kisiri / kimafumbo kuelekeza jamii wanamoishi.

## 2.6 Sababu za uchoraji vibonzo katika gazeti


Sababu ambazo huwafanya waandishi kushiriki katika uchoraji wa vibonzo ni nyingi. Kwanza, kuna wasanii wanaojichukulia kuwa wao ni wanasanaa kwa hivyo huchukulia kama uraibu wao. Hawa hujitambulisha kwa kuandika majina yao na huenda jina hilo likawa la utani tu kwa mfano aliyesifika sana ni Maddo,mwingine ni Gado na sasa tuna Igah kwenye gazeti la *Taifa Leo* nchini Kenya, wote wakiwa na nia ya kuwasiliana. Wengine hujiona kama wanamapinduzi kupitia kwa kazi zao, na kuna wale ambao huchora ili kujifurahisha tu na wengine ni dhana ya kisaikolojia kuichukulia kuwa namna ya pekee ya kuwasiliana.
Kuna wale wanaoshiriki katika uchoraji wa vibonzo kama namna ya kujipa ajira. Mfano mwafaka ni kutoka katika gazeti letu la *Taifa Leo.*Igah anachora na kupata njia ya kujikimu kimaisha hivi ni kwamba yeye hupata malipo yake kutokana na kazi hiyo.

Kimsingi vibonzo ni viwakilisho vya sauti za wanajamii.Wanajamii hutumia vibonzo kutolea maoni, mawazo au jumbe kuhusu maisha. Hivi ndivyo hali ilivyo magazetini. Wachoraji hao wamemulika jamii kwa kutumia vibonzo. Katika harakati hizi, wabunifu hao wanachukulia kwamba huenda viongozi wakaweza kuyabadili mienendo yao baada ya kuwapiku kwenye magazeti hayo yanayo chapishwa kila siku.

Ni dhahiri kuwa vibonzo ni namna ya mawasiliano ya kipekee ambapo waandishi huchora kuonyesha mawazo na hisia zao bila kuongea kwa kumulika jamii. Lengo lao halisi likiwa ni kupitisha ujumbe fulani yanayowakumba wanajamii lakini kwa njia ya ucheshi kwa kupitia vibonzo hivi.

Katika harakati hizi, wachoraji vibonzo wanachukulia kwamba huenda viongozi wakaweza kubadili mienendo yao baada ya kusoma magazeti hayo yanayowapiku na kuleta mabadiliko fulani.


Mfano; Vibonzo # 9, # 16, # 26, # 27, # 33





Kibonzo #9, hiki kinaonyesha jinsi ambavyo viongozi wanavyovuja pesa za kaunti kwa kujinufaisha wenyewe. Wanaiba pesa ya umma kwa kupeleka kwenye benki zao za nje na zingine kuwapa rafiki zao licha ya wanakandarasi kuleta zabuni zao.





Kibonzo # 16, kilichoko hapo juu, kwanza mhusika amepewa sura ya mnyama ambaye ni fisi.Bila shaka kinaashiria ulafi na tamaaya pesa kwa kuwa ni kiongozi wa Kaunti ambaye ana majukumu ya kuwashughulikia wananchi wake ipasavyo lakini wapi.Picha hii inakashifu viongozi wetu walio na tamaa nyingi ya pesa.




Kibonzo #26, hiki kinaonyesha namna ambavyo serikali inavyokandamiza wahabari kwa kutotaka waangazie mambo wanayofanya.Wanahabari hapo juu wanakatwa na shoka kwa kupitisha bili itakayo wanyamazisha kabisa. Hawana uhuru wa kujiamulia ni nini hasa watakachochora au kuandika kwenye magazeti




Kibonzo #27, inaonyesha miaka hamsini baada ya uhuru. Mkenya wa kawaida hana habari kuhusu miaka hamsini hajui atasheherekea vipi kwani angali anaishi kwa hema, mvua ndiyo hiyo kuwanyeshea kila siku lakini anasikia mlio wa ndege angani hana habari kwa nini.




Kibonzo # 33, ‘wanjiku’ mwananchi wa kawaida ana sahani yake ikidhania kuwa huenda hiyo ndege ikamwangushia angalau kitu kwa sahani yake. Kule kwa ndege kuna wakubwa ambao wanajadiliana jinsi mbavyo watagawa pesa inayotengewa watu mashinani kutumia. Hapa tunaangazia ubadhirifu wa pesa za umma bila kumjali anayemshughulikia ambaye ni mwananchi.

**Hitimisho**

Katika sura hii, suala zima la vibonzo limejadiliwa kuanzia historia yake, maendeleo yake, na ukuaji wake hadi sasa. Ni dhahiri kuwa vibonzo huwakilisha sauti ya mwananchi hasa katika jamii ambayo inaendeleza dhuluma. Mwananchi huwa anatumia vibonzo kuondoa shinikizo linalotokana na kusoma magazeti.Vibonzo hujishughulikia masuala ibuka katika jamii bila mipaka.

Imedhihirika kuwa wachoraji wa vibonzo wana ubunifu wa hali ya juu kutokana na uhuru wa matumizi ya lugha walionao. Vile vile, imedhihirika kuwa vibonzo ni vya aina tatu na hatuwezi kuziwekea mipaka sanaa hii.

# SURA YA TATU

## 3.0 MAUDHUI KATIKA VIBONZO KWENYE GAZETI LA *TAIFA LEO*

### Utangulizi

Katika sura hii, tumeainisha data katika makundi kamaudhui na kubainisha ni maudhui gani yanatawala katika vibonzo vya gazeti la *Taifa Leo.* Katika utafiti huu, tunachunguza jumbe ambazo zimejitokeza katika vibonzo kwenye gazeti la *Taifa Leo*. Jumbe hizi tunaziainisha kimaudhui kama ilivyo kwenye jedwali 1 lifuatalo. Maswala yanayojitokeza katika michoro hizi ni: Siasa, Ufisadi, Ukosefu wa Usalama, Ukabila, Elimu, Uchumi na Kazi. Lengo letu katika kugawa maudhui haya yamekuwa kubainisha maudhui ambayo yanatawala katika vibonzo hivyo kutoka kwenye gazeti la *Taifa Leo*. Tumefanya hivi kwa kutumia asilimia ya matokeo

## 3.1 Jedwali 1: Uainishaji ya Maudhui

**Vibonzo** **Maudhui**

| Vibonzo | Siasa | Ukabila | Ufisadi | Ukosefu wa Usalama | Elimu | Uchumi na Kazi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | ✓ | | | | | |
| 2 | ✓ | ✓ | | | | |
| 3 | | | | ✓ | | |
| 4 | ✓ | ✓ | | | | |
| 5 | | ✓ | | | | |
| 6 | | | | ✓ | | |
| 7 | | | | | ✓ | |
| 8 | | | | | ✓ | |
| 9 | ✓ | | ✓ | | | |
| 10 | | | ✓ | | | |
| 11 | ✓ | ✓ | | | | |
| 12 | | | | ✓ | | |
| 13 | | ✓ | | | | |
| 14 | | | | ✓ | | |
| 15 | | | ✓ | | | |

| | **Siasa** | **Ukabila** | **Ufisadi** | **Ukosefu wa Usalama** | **Elimu** | **Uchumi na Kazi** |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **16** | ✓ | | ✓ | | | |
| **17** | | ✓ | | | | |
| **18** | | | ✓ | | | |
| **19** | ✓ | | | | | |
| **20** | ✓ | | | ✓ | | |
| **21** | | | | | ✓ | |
| **22** | | | | | ✓ | |
| **23** | | ✓ | | | | |
| **24** | | | | | ✓ | |
| **25** | | ✓ | | | | |
| **26** | | | | | | ✓ |
| **27** | | | | | | ✓ |
| **28** | | | ✓ | | | |
| **29** | | | | | | ✓ |
| **30** | | | | ✓ | | |
| **31** | | | | | ✓ | |
| **32** | | | | ✓ | | |
| **33** | | | ✓ | | | |
| **34** | ✓ | | | | | |
| **35** | | | | | | |
| **36** | | | | | ✓ | |
| **37** | | | | | ✓ | |
| **38** | | ✓ | | | | |
| **39** | | | | ✓ | | |
| **40** | | | | ✓ | | |
| **41** | | | ✓ | | | |
| **42** | | | | | | |
| **43** | | | | | | |
| **44** | | | ✓ | | | |
| **45** | | | | | | |
| **46** | | | ✓ | | | |
| **47** | | | | | | |
| **48** | | | ✓ | | | |
| **49** | | | | ✓ | | |
| **50** | | | | | | |
| **Frikwenzi** | **10** | **08** | **13** | **10** | **06** | **03** |
| **Asilimia** | **20%** | **16%** | **26%** | **20%** | **12%** | **06%** |

## 3.2 Matokeo na Maelezo

Uainishaji wa jumbe kimaudhui umefanywa katika jedwali 1. Tunaziainisha jumbe hizi katika makundi sita kama ifuatavyo ; Siasa, Ufisadi, Ukosefu wa Usalama, Ukabila, Elimu, Uchumi na Kazi. Kutokana na uchanganuzi wetu, data ya makundi haya ya kimaudhui ni kama ifuatayo;

| Kielelezo 1; | Asilimia za Maudhui |
|---|---|
| Ufisadi | 26% |
| Siasa | 20% |
| Ukosefu wa Usalama | 20% |
| Ukabila | 16% |
| Elimu | 12% |
| Uchumi na Kazi | 06% |

### 3.2.1 Maudhui zilizoko katika uchanganuzi ni pamoja na:


a) Siasa
b) Ukabila
c) Ukosefu wa usalama
d) Ufisadi
e) Elimu
f) Uchumi na Kazi

### 3.2.1. Ufisadi

Kulingana na matokeo haya, inadhihirika katika data yetu, asilimia kubwa ya matokeo kuhusu ufisadi ambayo yameongoza kwa asilimia 26% .

Ukweli huu unaelezwa na mifano hii;

Vibonzo # 6 # 9, # 10, #16 # 18 # 20, # 34




Katika kibonzo # 9, kinadhibitisha ukweli kuwa ufisadi ni kitu kinachoendelezwa na viongozi. Katika kibonzo hiki i wazi kuwa Gavana huyu anapora pesa ya kutumika katika kaunti yake. Gavana huyu hataki kuwalipa wananchi wanaotaka kulipwa lakini pesa anazo za kuwapa. Wananchi wamepiga foleni ili waweze kulipwa kandarasi waliokwisha himiza lakini wapi kisingizio ilioko pale ni kuwa ado hakuna pesa. Kuongezea anawalipa rafiki zake.





Katika kibonzo #10, hapo juu, tunaona kuwa Gavana huyu anaombwa kuweza kulipa wanakamiti ya kaunti ili kuwanyamazisha. Hii ilitokea wakati ambapo hao ‘MCA’ kama watu wanao wahangaisha Magava la sivyo watawatoa nyadhifani. Pesa ya kutumiwa kwa mahitaji ya wananchi kwa kaunti wanataka kutumiya kuwanyamazisha maofisa.





Kibonzo # 6, kinaonyesha jinsi walinda usalama barabarani wanavyo vyonza pesa kwa wananchi. Ni dhahiri kuwa wanapoona gari lolote kwao wanaona benki ya pesa. Tazama 'ATM' kisha yule ofisa anayewasiliana na mwenzake kuwa akaribie 'Mpesa'.





Kobonzo # 18, kwanza kabisa kimepewa sura ya fisi, kuonyesha mwenye tamaa, na ni tamaa ya pesa. Anaonekana Gavana ambaye angependa bajeti ya Kaunti kuongezewa hela ndiyo wapate za kuiba. Huu ni uwizi wa hali ya juu hata mkoba wake umejaa na pesa hata zinavujwa tu nje.





Kibonzo #18, mwananchi huyu hajui la kujivunia kwa sababu pande zote ufisadi umekithiri. Yote yakiwa yanazorotesha uchumi wa Kenya. Hii ni hisia ya wananchi wengi kwa kuwa wasanii huchora vibonzo kulingana na kinachoendelea kiwakati.





Kibonzo #23, Kenya kusherehekea miaka hamsini licha ya wananchi wake kuwa wakimbizi wa ndani kwa ndani. Kwao hawaelewi lina maana gani kwa kuwa wangali wanaishi kwenye kampu bila makao, mvua na baridi tele, lakini mwenye shibe hajui njaa, wananchi hao walisahaulika ndiyo maana suala hili  linaangaziwa.





Kibonzo #28, viongozi hawa wamefilisi hazina ya pesa ya mashinani. Hapa mwananchi wa kawaida amewachiwa sahani tupu bila chochote. Picha hii inaonyesha jinsi viongozi hawajali kama watu wao wamepata hela zao.





Kibonzo #33, hii ni picha halisi ya nchi yetu, ‘wanjiku’ kama wanavyowaita wakenya wa kawaida hana hata nyumba lakini ansikia ndege ya mkubwa ikipita akitarajia huenda akajaliwa kupata kitu kwenye sahani. Wale wakubwa walioko juu wanajadiliana jinsi ambavyo watakavyogawana pesa inayotarajiwa kwenda kwa mwananchi pale mashinani. Kwao wanasema mashinani ni popote hata pale walioko juu ni mashinani. Jambo linalozorotesha sana maendeleo ya nchi.




Kibonzo #42, kinaonyesha mweshimiwa anapewa tunu kwa kuwa mlafi, yaani anaongoza katika kila aina ya ufisadi na anayempa medali pia ni kama yeye kuwa ni nguruwe anayekula kila kitu.Mwananchi wa kawaida yuko pale kando anashangazwa na jinsi walafi hawa wawili wakitunukiana medali ya kufuja mali ya umma.




Kibonzo # 44, Gavana huyu hana aibu kamwe, amezidiwa na tamaa ya pesa ambazo wananchi hawajui alipeleka wapi, mwili wake ukiwa unaningi’iniya na tamaa tu.




Kibonzo # 46, tunamwona mwenyekiti cha Hazina Ya Kitaifa yumo taabani, maadamu wabunge,magavana, 'MCA' wote wanataka nyongeza kwenye bajeti yao.Wamechorwa kuwa ndege walioko mawindoni ikiwa wana nia ya kumwangamiza.Wote wakitaka pesa zaidi kutokana na ubinafsi walio nao viongozi hao.

Vibonzo vingi vina maudhui ya ufisadi kwani matokeo yake yanachukua nafasi ya kwanza. Masuala ya ufisadi katika jamii imeshika usukani.
Kutokana na mifano hii ni wazi kuwa hii ndiyo taswira halisi ya jamii.Vile vile , ni wazi kuwa watu wengi katika jamii wanateseka kutokana na namna viongozi wanavyonyakua fedha za umma kiholela.Vibonzo hivi vilichorwa kwa sababu msanii anatatizika kuona jinsi ambavyo uchumi wetu umezorota kwa minajili ya ufisadi.Ni jambo la kusisitisha kutambua kuwa viongozi kama Gavana wa Kaunti ndiye ako kipawa mbele kushiriki katika ufisadi tena hajali walioko mashinani kwa kuwa wanazingizia kuwa hakuna fedha wa kulipa watu pamoja na wanakandarasi Pesa ziko tena ijapokuwa zinapita kandokando kwenye benki za kibinafsi.


Tunaweza kusema kwamba maudhui ya ufisadi yametawala kwa sababu jopo zilizowekwa kupambana na kupiga msasa ufisadi ndio wanaopatikana na donda hilo hilo.

### 3.2.2. Siasa

Maudhui kuhusu siasa vile vile yanavutia .Vibonzo vingi vinadhihirisha haya, kwani matokeo yake yanachukua nafasi ya pili kwa asilimia 20%. Masuala kuhusu siasa ni kiashirio cha kuwa nchi ya Kenya imemakinika katika siasa yao. Siasa ya kimataifa na kitaifa yote

yameangaziwa.Wabunifu wa vibonzo wanaonekana kuwa watu makini na wanafuatilia matukio ya kisiasa kadri yanavyopita.Ingawaje hawakuonyesha ni pande gani hasa wanaoegemea kwa kuwa katika kazi wanakashifu utawala mbaya.Tukitazama hapo juu tunaona namna ambavyo viongozi wanajishughulikia mambo ya siasa hasa mambo ya kampeni na kura a hapa na pale.Siasa za kitaifa zinaonekana kuongozwa na ukabila na chuki. Kitu ambacho kinazua dhana ya chuki miongoni mwa wananchi wa Kenya kwa kuwa kila mwamba ngoma huvutia kwake. Wasanii wanakashifu mienendo mibaya ya uongozi na kutaka wabadili mielekeo yao.

Mifano ifuatayo ni mwafaka; Vibonzo #1, #2, # 19, # 34




Kibonzo # 1, kiaangazia suala la uchaguzi.Msajili wa vyama anapatwa na mshangao kuwa kua yule ambaye anataka kuandikisha My dress my choice kama chama maadamu inawafuasi wengi. Kuna kuwa na ugumu fulani kwa sababu wakati huu ilipata kama kina mama wanadhulumiwa kutokana na mavazi yao. Kuna maandamano kutokana na suala hili lililozoa majadiliano kote nchini.




Katika kibonzo hiki, ni dhahiri kuwa mwanahabari anamhoji Mheshimiwa kuhusu mambo ya siasa, ndiposa anamuliza kuhusu msimamo wake kuhusu ‘vision 2030’ naye anamjibu kwa kusema kuwa anajua tu kuhusu ‘vision ‘ ya miaka ya uchaguzi.




Kibonzo kilichoko hapo juu inaleta taswira ya siasa pamoja na ukabila.Mwananchi aliyejukwani anahutubia wananchi wawe na amani licha ya kuzingirwa na ukabila. Huenda anataka kura kutoka kwao ndiposa afanye hivyo.




Katika kibonzo hiki, ni wazi kuwa wakati ambapo wakenya hujipumbaza namna hii ni wakati ambapo uchaguzi uko karibu. Wakenya hawa wanajifanya ni rafiki ilhali ukweli ni kuwa ni maadui, kila mmoja akiwa amebeba kisu ya kumjeruhi mwenzake.







Kibonzo # 27, kinaonyesha namna familia hujiingiza katika siasa hata kutaka uhusiano wao kuisha kwa sababu tu ya siasa kila mmoja akiwa anaegemea katika chama chake juu ya ukabila.Tazama wanavyosemezana ‘Michezo imeisha. Uhusiano wetu umeisha!’





Kibonzo # inaonyesha jinsi ambavyo Mhesimiwa anavyofilisi hazina ya Kaunti. Mwenzake anampotosha kwa kuwa anamtaka wanyamazishe ‘ MCA’ ndiyo aweze kupata umarufu nao na wasiweze kumpinga. Hali hii  inazua swala la ufisadi miongoni mwa viongozi nchini.




Katika kibonzo hiki kiongozi huyu anatafuta kura ili awez kuchaguliwa na wananchi. Licha ya kutahadharisha watu kutotumia ukabila kutafuta kura, yeye mwenyewe anaendeleshwa na

ukabila. Ni kinaya kuwa ansema ‘Jihadhari na wanaotumia kabila kutafuta kura’ naye anafanya kinyume.





Chuki na Ukabila huenea sana wakati wa uchaguzi. Ni wazi kuwa kila mwamba ngoma huvutia kwake, hivyo basi wanasiasa wanatumia ukabila kuendesha kampeni zao.





Huyu kiongozi anunga mkono hoja ya kura ya maoni kuwa hela za Kaunti ziongezwe…ili apate za kuiba. Dhana ya siasa inajitokeza hapa. Huenda huyu ni Gavana au Seneta ambaye anatamaa ya kupata fedha ya kujinufaisha.

### 3.2.3. Ukosefu wa Usalama

Maudhui ya nafasi ya tatu ni ukosefu wa usalama ambayo yana asilimia 20%. Inaonekana kuwa wanavibonzo nchini wanasikitishia jinsi ambavyo usalama wananchi inavyoendelea kudorora. Hata polisi wa kulinda wananchi anahofia maisha yake na kutaka usalama wake kwa kujificha chini ya meza. Suala hili la ukosefu wa usalama umeangaziwa kwa kina kwa sababu wakenya wengi wanakufa kila uchao kutokana na magaidi kutoka nje. Kila wakati kuna mlipuko wa bomu na habari kwenye runinga na redio ni hizo tu, hata wananchi wamechoshwa na habari hizo. Tazama vibonzo vifuatavyo; #3, #6, #11, #30, #39, #49.





Taswira hii inatupa hali iliopo Kenya kuwa hakuna usalama tena. Tunaona hapo awali iliandikwa 'KARIBU KENYA HAKUNA MATATA' pembeni kuna mlipuko wa bomu hivyo hakuna utulivu tena na bango hilo liliweza kusoma KENYA KUNA MATATA. Hii inadhibitisha kuwa iwapo unataka kuja Kenya tahadhari kwa kuwa kuna ukosefu wa usalama.





Ni kinaya katika kibonzo hiki kuwa hata yule askari anayeangalia magari kwa minajili ya kuzuia chochote cha kuumiza mtu asiweze kufichwa, hana hata habari inafananaje. Hata dereva yule amebaki ameshangaa kweli.




Katika kibonzo hiki askari anakejeliwa kwa sababu anamfanyia msako mwanachi kutafuta silaha  aina ya panga na rungu naye amezibeba juu lakini hana habari hiyo kamwe isipokuwa yule anayemtazama kwa nyuma.




Kibonzo hiki kinaonyesha jinsi serikali anasumbuliwa na magaidi hapa na pale hapumui kamwe. Ni dhahiri kutokana na picha hii kuwa serikali inakabiliwa vikali na shida ya kuwazuia wagaidi kuingia nchini.Hakuna amani.




Hatari za kujivunia kuwa Mkenya iko wazi .Wanajamii wanahangaishwa kila pahali ikiwemo wanakoishi nyumbani, katika nyanja ya usafiri haujazazwa kamwe, vile vile katika mkahawani. Kuna mwananchi anayebeba jeneza kutoka kwa mkahawa kuonyesha kuwa maisha imekuwa magumu kila pembe ya nchi.





Kibonzo hiki kinaonyesha kuwa polisi wa kulinda wananchi ndio wa kwanza kuhofia maisha yao na kujificha chini ya meza na kutaka wanajeshi kuletwa ili nao pia walindwe, kinaashiria ukosefu wa usalama wa hali ya juu. Mwananchi wa kawaida atakimbilia nani iwapo polisi ameshatokomea.


### 3.2.4. Ukabila na Chuki

Maudhui kuhusu Chuki na Ukabila yamepata asilimia 16%. Maudhui haya yamefungamanishwa na siasa na kwa kiasi kikubwa chuki. Hivi ndivyo hali ilivyo nchini Kenya; siasa inaegemea upande wa makabila sana.Mifano tuliyopata kutoka kwa data yetuni kama ifuatayo;

Vibonzo # 5, # 12, # 17, # 23, #25, # 38.




Kibonzo hiki kinaonyesha namna ambavyo ukabila umekithiri katika mitandao. Hii inachochewa na chuki walio nao watu wenye kabila tofauti tofauti na huonekana sana wakati wa uchaguzi baada ya miaka mitano na kuendelezwa jinsi inavyoonekana. Jamii ya Wakenya wamegawika katika kabila mbalimbali na hii huleta hali ya uhasama katika nchi yetu.




Ni jambo la kusikitisha kuwa, kutokana na ukabila wananchi wa kenya huuana kutokana na tofauti za kisiasa na uongozi unao egemea upande huo huo. Hisia kwa mitandao inazidi kila uchao kwa sababu ya viongozi na damu inyoonyeshwa hapa ni damu ya wakenya wanaotofautiana juu ya ukabila na chuki miongoni mwao.





Katika kibonzo hiki, ni jambo la kusikitisha kuwa kiongozi huyo anazungumzia jambo kuhusu udugu ilhali ukabila umemvaa kotekote ya kuwaangamiza wale wasio wa kabila lake.





Wananchi hawa wanakejeliwa na wanavibonzo kuwa wanakumbatiana kuwa ndugu lakini kila mmoja amebeba kisu ya kumwangamiza mwenzake. Kibonzo hiki kinaonyesha jinsi jamii ya wakenya wanavyo hadaiana kwa kujifanya kuwa ndugu lakini ndani yao wanachuki ya kuuana.

### 3.2.5. Elimu

Elimu kama maudhui pia imeangaziwa kwa mapana. Tunaona kuwa wanafunzi wanalalamikia kutokuepo kwa kazi licha ya kujihusisha na masomo nyingi zenye changamoto katika chuo kikuu na wanapotoka huko hakuna kazi wanaishia kwenye ombwe tupu. Tazama vibonzo hivi; Vibonzo #7, #8, #21, #22, # 24, #31




Kibonzo hiki kinadhihirisha kuwa hakuna kazi. Swala la kazi lina changamoto humu nchini.Wengi wa wanafunzi hawaoni faida yoyote ya kuwa chuoni. Baada ya wanafunzi kuelimika wanatarajia kupata kazi. Ajira ndio matunda ya elimu. Ni kinaya kuwa hapa nchini tatizo la ajira ni sugu sana. Tazama vibonzo vilioko hapo chini.





Huyo mwanafunzi alihitimu na kupata shahada, lakini anakaribishwa wapi pa kupata kazi. Magaidi ndio wanamkaribisha kuwa kuna kazi ya ugaidi. ‘ Karibu ndani’, ‘Alshabaab was here’ haya ndiyo maandishi yaliyoko pale. ‘ HAKUNA KAZI’ iko pale kwa mlango. Hajui afanye nini ndiyo apate ajira.




Kupata kazi nchini sio rahisi. Kibonzo hiki kinaonyesha jinsi ambavyo wakenya wengi huenda kujitafutia ajira Saudi Arabia lakini wanaporejea hao hurudi kwa jeneza, kutokana na mateso wanayopata huko. Wengi huuawa na matajiri hao ambao waliwaajiri  kutopatana, hakuna uhuru wowote huko wa kujiamulia chochote ila madhila na mateso chungu nzima.




Mwanafunzi huyu katika kibonzo kilichoko hapo juu ,analaumu mgomo ya walimu kumfanya asifaulu.




Mwanafunzi huyu ameathirika kutokana na teknolojia ya kisasa, kwa kuwa hawezi jibu maswali ya mtihani aliyopewa, jambo ambalo linakumba sekta ya elimu nchini.




Katika kibonzo hiki mwalimu anashurutishwa na serikali kuweka sahihi kwenye mkataba kuwa hawata goma tena, lakini tunaona kuwa mwalimu hatishiki hata na bastola kichwani hatingisiki kuitia sahihi, jambo ambalo hata wakati huu tunashuhudia.




Walimu nao wanagoma kila uchao ndiposa hata mwanafunzi hawezi imba wimbo wa taifa ila kuimba wimbo ule wa walimu wa mgomo ‘Solidarity forever,’ Kibonzo # 7. Mwanafunzi kutofanya vizuri kwenye mtihani analalamikia mgomo





Katika kibonzo hiki, Chuoni  mhadhiri kumhadaa mwanafunzi na mapenzi ndiyo apewe alama zake ni uozo katika jamii. Haya yote yanaonyesha jinsi sekta ya elimu inavyokumbwa na changamoto ya aina hii.

### 3.2.6 Uchumi na Kazi

Hali ya Uchumi nchini Kenya ni ngumu. Wakenya wengi wanaenda nchi za nje kutafuta ajira, na kila wanapofika huko ni mateso chungu nzima na mwisho hurejea kwa jeneza. Kibonzo # 43, # 36, na tena wasomi wanakaribishwa katika genge la magaidi kwa kuwa kazi hakuna humu nchini.Walimu wanagoma kila mara kutokana na ugumu wa maisha, hata

huabidi kufanya kazi mbadala ili waweze kujikimu.Uchumi wa Kenya inadorora kwa sababu watu wengi hawawezi kujimudu kimaisha ingawaje sirikali inasheherkea miaka hamsini tangu kupata uhuru wao.Wakimbizi wa ndani kwa ndani angali wako kwenye kampi na hakuna anayewakumbuka. Kibonzo # 27, # 43, .Viongozi wanatamaa nyingi ya kujitajirisha hata wananyakua pesa zinazoweza kuwasaidia watu mashinani.




Katika kibonzo hiki, Kenya  kama nchi inasherehekea miaka hamsini. Kinacho tupa wasiwasi ni kuwa walioko kwenye hema hiyo kama wanahabari hiyo. Fedha nyingi zinatumiwa kwa matayarisho ya kusherehekea lakini uchumi wetu umezorota sana mwananchi wakawaida hawezi kujimudu.




Kazi inapokosekana, wananchi wanatafuta ajira Saudi Arabia, lakini wanaporudi wao hurejea na jeneza. Wengi huenda huko na kurudi kwa jeneza kama ilivyo kwenye kibonzo hiki. Kwa kuwa ‘Wanjiko’ anatafuta namna ya kujikimu maadamu hali ya uchumi iko juu bila shaka wao hufanya wawezekanavyo kuweza kuishi.

**3.2.7**

Kutokana na data ni dhahiri kuwa maudhui kuhusu Ufisadi, Siasa, na Ukosefu wa Usalama yanatawala katika vibonzo vya gazeti la *Taifa Leo* katika kipindo hicho.


Matokeo haya yanakubaliana na madhumuni ya utafiti huu kwamba maudhui ya Ufisadi na Siasa yanatawala katika vibonzo hivyo vya *Taifa Leo*.

Katika kuhitimisha, ni muhimu kutaja kuwa kuna vibonzo ambavyo vilikuwa na maudhui ambavyo yalikuwa zaidi ya moja.. Kwa mfano ;

Kibonzo # 2 ,




Kibonzo hiki, kina maudhui zaidi ya moja. Kwanza kunawalinda usalama pale kuonekana kuwa mwingine anawazia bomu au gurunedi pahali. Kuna chuki katika kibonzo hiki. Kuna mtu ambaye anawasiliana na mtu na tunapata kuwa anaandika 'CHUKI'. Huenda pia kuna dhana ya ukabila kwenye mtandao. Kuna kijana kule ndani ambaye anaendeleza chuki kwa njia ya mtandao.





Kibonzo # 20, ina maudhui ya ukabila pamoja na siasa. Hii ni kwa sababu ni wakati wa kampeni na viongozi wengi wanatafuta kura kwa wananchi. Aidha wanatumia kabila kutafuta

kura ndiposa tunamwona huyu kama amebebwa na kabila lake ili kutafuta kura kutoka kwa wananchi huku akitadharisha wananchi.’ Jihadhari na wanaotumia kabila kutafuta kura licha ya yeye kufanya vivo hivyo.




Kibonzo # 27, kinadhihirisha maudhui ya ufisadi, uchumi na kazi pamoja na ubinafsi. Serikali za kaunti wanaiba pesa za Kaunti huku wakiwahadaa wananchi kuwa hakuna pesa. Jambo kama hili linafanya uchumi wa Kenya kufifia sana na watu kufa moyo kutokana na kutolipwa ilhali pesa hizo ziko. Tazama anapodanganya na kusema ‘ Subiri. Bado tunangojea pesa kutoka kwa Serikali Kuu.




Mkenya anayechorwa hapa, amezingirwa na kila aina ya uovu katika jamii yetu. Siasa, mfumuko wa bei, ukosefu wa usalama, njaa, Ukosefu wa kazi zote zinamwandama ndiposa anauliza swali la balagha ‘ Nitajivunia kuwa Mkenya? Ameandamwa na shida nyingi zinazotupa aina za maudhui kwa jumla.

Kutokana na uchanganuzi huu, misingi ya Nadharia ya Mawasiliano ya Utambulisho ya Giles imefaa sana kwani imesaidia kuonyesha utambulisho wa wanavibonzo kwa kupitia maudhui tawala. Ili kuonyesha utambulisho wa wanajamii fulani, kuna mambo kadhaa ambayo hufanana na ndio huwa kibainishi cha Utambulisho wao. Jamii wanaoangazia wanavibonzo ni jamii ya Wakenya kwa jumla. Tunapata kuwa maswala mengi ambayo yamejitokeza ni ya kijamii. Hivyo basi masuala ambayo yanaashiria Utambulisho ni wa kitaifa.

**Hitimisho**

Katika sura hii, imejadili maudhui katika vibonzo ambayo imetumika kwenye gazeti la *Taifa Leo*. Jumbe imeainishwa katika makundi yafuatayo; Ufisadi,Siasa, Ukosefu wa usalama, Ukabila, Elimu, Uchumi na Kazi katika vibonzo vya gazeti la Taifa Leo. Matokeo yaonyesha kuwa maudhui ya Ufisadi na Siasa ndiyo yanayotawala katika vibonzo hivyo.

# SURA YA NNE

## 4.0 MITINDO YA LUGHA ZILIZOTUMIKA KATIKA VIBONZO VYA *TAIFA LEO*

### Utangulizi

Katika sura hii, uainisha wa mitindo ya lugha zilizotumika kwenye vibonzo katika gazeti la *Taifa Leo* umefanywa, ili kubainisha ni mbinu gani hasa inayopendelewa sana.

Mathooko (2007), anasema kuwa lugha ni mfumo wa sauti nasibu zinazo kubaliwa kutumiwa katika jamiilugha fulani ya watu wenye utamaduni sawa kwa ajili ya mawasiliano.

Kutokana na ufafanuzi huu, sifa mbili kuhusu lugha ambazo ni muhimu katika uchanganuzi wetu nazo ni kuwa:

a) Lugha hutumiwa na jamii moja yenye utamaduni sawa.
b) Lugha ni chombo cha mawasiliano.

Katika hali iliyoko tumejikita katika muktadha wa gazeti hasa katika mazingira ya uchoraji wa vibonzo. Kwa hivyo, katika utafiti wetu, tumechukulia jamii kumaanisha watu ambao wanashiriki katika mazingira ya uchoraji vibonzo na wasomaji wa gazeti hili. Watu hao lazima huwa ni wakenya ambao wanajua shida zinazowakumba wakenya na kuathiri wao pia. Wanavibonzo wameshiriki katika kuchora kwenye magazeti kwa lengo la kuwasilisha jumbe tofauti tofauti kwa jamii kwa kutumia vibonzo.

## 4.1 Lugha kama chombo cha Mawasiliano

Ni dhahiri kuwa lugha na jamii ni vitu viwili ambavyo haviwezi kutenganishwa.

Nadharia tete ya Sapir na Whorf inadai kuwa, lugha ni kama chombo amilifu ambacho humwezesha binadamu kuufafanua utamaduni wake kwa msingi ya mazingira aishimo. Lugha basi inakuwa kama asasi ambayo mwanadamu huitumia kuwasiliana na kuhusiana na wanajamii wenzake.

Mawasiliano ni utaratibu wa kuhamisha ujumbe kutoka kwa mwasilishi hadi kwa mpokezi, kupitia kwa matumizi ya lugha . Buliba na wenzake (2006). Katika utafiti huu tunachukulia mawasiliano kumaanisha utaratibu wa kuhamisha ujumbe kutoka kwa vibonzo vya gazeti la

*Taifa leo* hadi kwa wasomaji wake, ( ambao ni hadhira lengwa) kupitia matumizi ya vibonzo vilivyoambatishwa na maneno.
Mbinu hizo zinazodhihirika ni pamoja na; Jazanda, kinaya, kuchanganya msimbo, kejeli, chuku, taharuki, n.k

## 4.2 Lugha kama Kitambulisho

Watu ambao wanajipata katika mazingira ya uchoraji vibonzo katika magazeti, huwa wanatoka katika jamii zenye jamii tofauti ya lugha.Wanasanaa wa vibonzo hao wanapokutana huwa kunatokea makutano ya lugha kama anavyosema Giles, kwani lazima wapunguze tofauti zao ili waweze kujihusisha na watu wengine katika jamii hii pana.
Hii ni kwa sababu, lugha huwapa binadamu Utambulisho wa hali ya kujihisi kwamba wao ni watu wa kushirikiana katika kufanya kazi pamoja kwa manufaa ya wote. Lugha inawaunganisha wanajamii na kuwafanya wajihisi kuwa wanathamini mambo mamoja. Kutokana na sababu mbalimbali za kimazingira na kijamii, jamiilugha moja yaweza kugawika katika lugha tofauti tofauti.

Maingiliano baina ya jamii tofauti za wanalugha mbalimbali yamesababisha hali ambapo mara nyingi haiwezekani kupata jamii ambayo ina umoja lugha. Jamiilugha pana inaweza kuwa na jamiilugha nyingi ndogo ndogo ndani yake kutegemea vigezo kama umri, tabaka, jinsia, taaluma, ajira na kadhalika. Hivi ndivyo hali ilivyo katika nchi yetu ya Kenya.
Katika maingiliano ya wanajamii waliopo katika jamii pana, haifai wazungumzaji lugha kupata shida katika matumizi ya lugha kwani wanajua ni lugha gani watumie wapi, wakati gani na kwa nini. Hivi ni kusema kuwa mtumiaji lugha anajua jinsi ya kutosheleza mahitaji ya kila siku.

Kwa namna ambayo Wasanii wa vibonzo hutumia ubunifu wao ili kuchora vibonzo vinavyo sawiri jamii na kuvutia wasomaji yao na wakati huo huo kupitisha ujumbe. Mitindo ya lugha inayojitokeza ni mingi na tunayaangalia kwa kila moja.

Uchanganuzi wa matini kimtindo hufanyika katika muktadha wa lugha. Simpson (2004), anaelezea kuwa lugha ni muhimu sana kwa wanaochunguza mtindo kwa sababu maumbo, ruwaza na viwango ambavyo ni sehemu ya muundo wa kiisimu ni muhimu sana katika

kudhihirisha uamilifu wa matini husika. Mbinu za kiisimu zenyewe huwa hazileti maana bila kufanyiwa uchanganuzi na kutoa fasiri kamili.

Katika jedwali 2, tunachunguza jumbe katika vibonzo kwenye gazeti la *Taifa Leo*. Suala la mitindo ya lugha ni pana mno lakini katika utafiti huu tunachunguza mitindo ya kitamathali, na ukiushi ambayo imejitokeza kwa wingi mno.

### 4.2.1 Jedwali 2; Mitindo ya lugha

| Vibonzo | Tamathali za usemi | Ukiushi |
|---|---|---|
| 1 | Kuchanganya msimbo | Sintaksia |
| 2 | Kuchanganya msimbo | Sintaksia |
| 3 | Kejeli | - |
| 4 | - | - |
| 5 | - | - |
| 6 | Kinaya | - |
| 7 | Kinaya | - |
| 8 | Kinaya | - |
| 9 | - | - |
| 10 | - | - |
| 11 | - | - |
| 12 | Kinaya | - |
| 13 | - | - |
| 14 | Taharuki | - |
| 15 | - | - |
| 16 | Jazanda | Semantiki |
| 17 | Jazanda | - |
| 18 | Kejeli | - |
| 19 | Uhuishi & Kuchanganya msimbo | Mofolojia |
| 20 | Kinaya | - |
| 21 | - | - |
| 22 | - | - |
| 23 | Kinaya & jazanda | - |
| 24 | Kuchanganya msimbo | Mofolojia |
| 25 | Kinaya | - |
| 26 | Balagha | Sintaksia |
| 27 | Kinaya | - |
| 28 | Chuku | Mofolojia |
| 29 | - | - |

| | | |
|---|---|---|
| 30 | Jazanda | - |
| 31 | - | - |
| 32 | Sitiari | Sintaksia |
| 33 | - | - |
| 34 | Jazanda | Sintaksia |
| 35 | Jazanda | Sintaksia |
| 36 | Kanaya | - |
| 37 | - | - |
| 38 | Kinaya | - |
| 39 | - | - |
| 40 | - | - |
| 41 | Kuchanganya msimbo | - |
| 42 | Jazanda | Sintaksia |
| 43 | - | - |
| 44 | - | - |
| 45 | - | - |
| 46 | Jazanda | Semantiki |
| 47 | Uhuishi & kuchanganya msimbo | Semantiki |
| 48 | Kinaya | - |
| 49 | Jazanda | Semantiki |
| 50 | Ukiushi wa Herufi kubwa | - |

**Tanbihi**

Katika jedwali hili, kuna sehemu ambazo zina mapengo. Mianya hii inawakilisha jumbe ambazo wasanii wake hawakutumia mitindo yoyote ya lugha tunayoishughulikia ambayo ni ya kitamathali.

### 4.2.2 Lugha ya kitamathali kama mtindo

Tamathali ni neno au kifungu ambacho kina maana iliyofichwa, (Wamitila 2003). Tamathali ni mojawapo ya mbinu za matumizi ya lugha ya mkato nay a kisanii. Tamathali hizi humwezesha mtunzi kusema mengi kwa maneno machache yenye mvuto, mguso, na mnato. Tamathali za usemi ambazo tunazishughulikia ni pamoja na ; Jazanda, sitiari, kinaya, kejeli, chuku, pamoja na kuchanganya msimbo. Tumechagua tamathali hizi kwa sababu uchanganuzi wetu umeonyesha kuwa tamathali hizi zimetumiwa kwa wingi katika vibonzo hivi vya *Taifa Leo.*

Tumezijadili tamathali hizi kama ifauatavyo;

a) Sitiari

Mbatia (2000), anaeleza sitiari kama ulinganishi usio wa moja kwa moja kwani hautumii viunganishi vya ulinganishi kama vile, mithili ya, ja, au kama.

Msokile (1993), anatoa ufafanuzi wake kwa kusema kuwa sitiari ni tamathali ya usemi inayolinganisha au kuhusisha vitu vilivyo tofauti kwa kitabia au kimaumbile. Msokile anaendelea kusema kuwa , vitu au viumbe viwili vilivyo tofauti kitabia au kimaumbile iliyopo kati ya vyote viwili ama zaidi bila ya kutaja dhahiri sifa hiyo.

Kwetu, dhana ya sitiari yanamaanisha ulinganishi wa vitu viwili na kuvifanya vionekane kama vyenye sifa za kufanana ilhali vitu hivi ni tofauti kabisa. Kutokana na utafiti wetu, sitiari imetumika ingawaje si kwa wingi. Mfano tunaipata katika vibonzo hivi;

Kibonzo # 32 & # 43




Muhubiri hapa analilia kupewa silaha ya kuweza kujikinga kwa sababu madhehebu wamekuwa wakiuliwa sana, na hili lilitokea wakati wa ukosefu wa usalama ulivyokithiri sana

nchini, kwa hivyo wembe hapa kinafananishwa na bunduki. Hakika walitaka wapewe bunduki.




Kwa kuwa kupata ajira nchini Kenya ni nadra, wananchi wengi huenda kuitafuta ughaibuni, na wanapo rejea, hurudi kwa jeneza. Maisha huwa ni magumu huko na kuteswa na wanaowajiri huku. Hapa kazi imeweza kufananishwa na jeneza huko Saudi Arabia.


b) Jazanda

Mbatia (2000), anaeleza kuwa jazanda ni kunga ya utunzi ambapo lugha inatumia kusawiri picha fulani kutokana na maelezo yanayotumia maneno teule au tamathali za usemi. Kwa njia hii mtunzi anamwezesha msomaji kuona, kuhisi kitu kinachoelezwa.


Mifano; Vibonzo # 16, # 17, # 34, # 35, # 42, # 49





Katika kibonzo hiki, mwanasiasa huyu amepewa sura ya fisi kuashiria tamaa na ulafi wa fisi. Maneno anayotamka yanadhihirisha haya ‘Naunga mkono hoja ya kura ya maoni kuwa hela za Kaunti ziongezwe….ili tupate za kuiba’.Kwa hivyo viongozi wetu hawajasazwa kutokana na tabia ya kuiba pesa za umma.




Katika mchoro huo hapo juu hiyo mapu ya Kenya ni taswira ya Wakenya. Kisu hicho kinaonyesha jinsi ambavyo Wakenya wanavyouana kutokana na hisia zao kwenye mtandao. Ni ishara ya chuki kote kote nchini na tunaona damu ikiwa imetandaa kila pahali chini.




Kibonzo # 32, kinaonyesha uwanja wa wanadondi. Jambo la kushangaza ni kuwa wanadondi hao ni Serikali na Wanahabari. Hii ni vita inayoonyesha namna ambavyo Serikali imekuwa ikawanyamazisha wanahabari kwa kupitia bili waliopitisha kuwa hawatakubaliwa kuchapisha bila idhini ya Serikali. Jambo hili lilizua hisia mbalimbali nchini wakati huo.




Anayejivunia kuwa Mkenya ni aina ya mnyama Fisi na anayemvisha tunu pia ni mnyama aina ya Nguruwe. Mkenya wa kawaida anapatwa na mshangao kuwaona hawa wanyama wawili wanavyoendeleza dhana hii. Hawa ni kiashiria cha viongozi wetu nchini. Sifa zao ni Ulafi, Rushwa, Hongo,na Kiinua mgongo. Licha ya haya yote angali anasema, 'Najivunia kuwa Mkenya.




Kwa kuwa kupata ajira nchini Kenya ni nadra, wananchi wengi huenda kuitafuta ughaibuni, na wanapo rejea, hurudi kwa jeneza. Maisha huwa ni magumu huko na kuteswa na wanaowajiri huku. Hapa kazi imeweza kufananishwa na jeneza huko Saudi Arabia.

c) Chuku

Kulingana na Wamitila (2003), chuku ni hali ambayo sifa fulani hukuzwa kupita kiasi. Naye Mbatia (2000), anasema kuwa chuku ni matumizi ya lugha ili kutilia chumvi kitu au hali fulani aghalabu kwa madhumuni ya kusisitiza. Tamathali hii hutumika kuikuza sifa fulani kupita mipaka. Lengo kuu la kulitumia chuku ni kulifanya jambo au kitu kionekane kwa udhahiri zaidi. Kwa mfano: Kibonzo # 12, anatilia mkazo ukosefu wa usalama nchini.




Linasikitisha kwamba maafisa ambao wanatarajiwa kuwalinda wananchi ndio wanahofu zaidi kuhusu mashambulizi nchi hadi nao kujificha kuta kulindwa pia na masoja.Haya yote yamejitokeza kwa kuongezea chumvi mno hasa wanapoitisha ulizi huo kila wakati.




Ni jambo la kushangaza kupata kuwa mwalimu anamwambia mwanafunzi kuimba wimbo wa taifa, lakini mwanafunzi huyu hawezi kuimba wimbo huo na badala yake anaimba wimbo ule huimbwa na walimu wanapo goma. Kuashiria jinsi ambavyo migomo ya walimu umekuwa na athari kubwa kwa wanafunzi.’ Solidarity forever,…Solidarity forever…’


d) Balagha

Hii ni matumizi ya maswali ambayo majibu yake kwa kawaida yanakuwa yameeleweka na hayahitaji kujibiwa, Msokile (1993).

Kwa mifano; Vibonzo # 20, # 41.

Vibonzo hivi vinaonyesha jinsi ambavyo mwananchi anavyokumbwa na matatizo chungu mzima kuwa Mkenya hata maisha hawezi kujikimu. Kingine kinaonyesha namna ambavyo Wakenya wanaofanya katika baraza la jiji si wafanyi kazi wa kweli huenda wakawa ni mizuka tu wanaolipwa mishahara ya bure ndiposa mwingine anauliza mwezake iwapo naye atafutwa kazi.




Kibonzo kinaonyesha Mkenya ambaye amekumbwa na shida si haba, sio siasa duni,mfumuko wa bei, usalama, njaa, ukosefu wa kazi. Je anajiuliza iwapo bado atajivunia kuwa Mkenya. 'Nitajivunia kuwa Mkenya?' Ni swali kweli halihitaji majibu.

e) Ukiushi kama Mtindo

Neno ukiushi katika lugha lilitumika kwa mara ya kwanza na mwanaisimu wa shule ya Prague kwa jina Mukarowsky (1982), kueleza namna lugha ya kifasihi inaweza kutofautiana na matumizi ya kawaida ya lugha. Thornborrow na Wareign (1998).

Neno ukiushi linatokana na neno kiuka linalomaanisha fanya sivyostahili, vunja sheria au fanya makosa. Shake (1991), anaendelea kusema kuwa, maingiliano yoyote yanayoathiri lugha kimuundo, kisarufi na hata kimsamiati ambayo yanazivunja sheria za lugha hiyo ni ukiushi wa kimatumizi.

Naye Mbatia (2000), anasema kuwa ukiushi ni uvunjaji wa kimakusudi wa kaida za matumizi lugha ili kubuni njia mpya za kujieleza . Hii inamaanisha kuwa msanii anatumia mbinu hii ya ukiushi kuzivunja sheria za matumizi ya lugha ili kupata malengo yake katika kazi ya kifasihi.

Ukiushi katika utafiti huu inauchukulia kuwa kanuni za lugha sanifu uwe wa kimaksudi au bila kujua; Lugha za Kiingereza na Kiswahili katika muktadha wetu. Ujuzi na elimu tuliyo nayo ya lugha imetuwezesha kuyatambua makosa ya kisarufi ili kubainisha ukiushi katika matumizi ya lugha.

(i) Ukiushi wa Kimofolojia

Huu ni uvunjaji wa kanuni zinazo tawala uendelezaji wa maneno kama vile; urefushaji wa maneno na ufupishaji wa maneno.

Kwa mifano; Kibonzo # 24




Katika kibonzo hiki ni wazi kuwa neno ambalo limefupishwa ni ‘sms’ ambalo kwa urefu ni Short Message Services.Vile vile tunapata kuwa yameandikwa kwa herufi ndogo ambalo linaleta ukiushi wa herufi kubwa kwa neno. ‘Sasa hii nitajibu kwa sheng ama kama sms. Mwanafunzi huyu hana uelewa wa yale ambayo anafanya katika mtihani huu.




Sentensi kwenye kibonzo hiki kina ujumbe ‘ Karibia Mpesa. Natuma saa hii. Kiashiria cha ‘Mpesa’ ni ‘Mobile Pesa’ ni njia mmoja wapo wa kutuma pesa kwa kutumia rununu na pale tena tuna pata ‘ATM’. Kinashiria ‘Auto Teller Machine’ ni mashini inayotumiwa kutoa pesa kwa njia ya kadi.

(ii) Ukiushi wa Kisintaksi

Huu ni ukiukaji wa kanuni za mpangilio wa maneno katika sentensi au kukosa upatanisho wa kisarufi. Kwa mfano;

Ujinga sasa imeingia badala ya ujinga sasa umeingia

Nyingine ni ukiushi wa kisemantiki ambayo ni matumizi mbali mbali ya mbinu za lugha yanaweza kufanya neno likachukua maana ambayo ni tofauti ya kawaida.

Kwa mfano, neno kuruka kuwa na maana nyingine isiyo tambulika.

Kuruka kumanisha kwenda densi

Aidha tuna ukiushi wa kifonolojia, na katika aina hii ya ukiushi, uandishi wa maneno huwa katika msingi wa kifonetiki au kifonolojia. Mifano ;

Nipeko badala ya nipe. Kulako badala ya kula n.k

f) Tabaini / Ukinzano

Msokile (1993) anasema kuwa tabaini ni matumizi ya maneno yanayokinzana.

Kwa mifano ; Vibonzo # 11, # 23, # 25 # 38




Kibonzo #11, kinaleta dhana ya ukinzani kuwa msemaji anasema ‘ Tunaishi kama ndugu na dada’ lakini si kweli hivi kwamba kivuli chake kinaonyesha mtu anayeukabila, na amebeba upanga wa kumwangamiza huyo anayemwita ndugu na dada.




Kibonzo hiki , kinaonyesha watu wanaojivunia kuwa pamoja wakati wanariadha wanashinda mbio kwenye runinga. Inapofika wakati wa siasa kila mmoja anavutia kwake wanasemezana ,'Michezo imeisha. Uhusiano wetu umeisha'.




Katika vibonzo vilioko hapo juu ni bayana kuwa yale wasemavyo sivyo ndivyo bali maneno yao yanakinzano ya kila aina. ' Tuombee amani nchini', lakini kila, mmoja amebeba kisu cha kumwangamiza mwenzake.


g) Kinaya

Ni kutendenda kinyume cha matarajio. Kama vile viongozi wengi kuiba pesa za umma badala ya kuwasaidia .Pesa mashinani inkuwa pesa kwa mfuko.

Mifano, Vibonzo #11, # 15, #26, #28 , # 33.




Ni kinaya kuwa mhadhiri ambaye anatarajiwa kumpa mwanafuzi mwelekeo ni anayemwonyesha mapenzi. Anamhadaa mwanafunzi huyu kuwa mtihani ni rahisi iwapo tu atakubali mwito wake.’ Mtihani wa leo sio mgumu’ na huku anampangia uroda.




Katika kibonzo hiki, ‘ wanjiku’ anatumaini kuwa huenda hiyo ndege ikampa kitu kwenye sahani ilyotupu. Vingozi walioko pale kwa ndege wanajadilianan jinsi ambavyo wataweza kugawanya pesa za kutumika mashinani. Wanasema’ Mashinani ni popote. Hata hapa tulipo’. Mwenzake akimjibu kuwa, ‘Hilo ni wazo nzuri. Nipe zangu’. Hawa watu hawajali maslahi ya wananchi waliowaweka kwenye hivyo vyeo vyaa juu, wanaubinafsi tu kwa kuwa kil akitu ni kujinufaisha tu.

h) Kufupisha maneno

Hapa tunaona Akronimu kama imetumika, lengo likiwa ni kuonyesha ubunifu wao na kuvutia wasomaji lengwa.


Mfano; 2 Kibonzo # 10. MCA badala ya Members of County Assembly.




Kibonzo # 15. ATM badala ya Auto Teller Machine na Mpesa- Mobile Pesa




Kibonzo # 19. R.I.P badala ya Rest In Peace





i) Dhana ya uhuishi pia imeweza kujitokeza katika vibonzo vingine. Tunaona wasanii kuwaweka wafu kuwasiliana wakiwa kaburini licha ya hao kuwa wafu. Marehemu ya kwanza aliaga kabla ya uchaguzi wa 2007 na wa pili punde tu baada ya uchaguzi wa 2007, wakati ambapo palizuka rabsha baada kura kupigwa.

j) Kuchanganya msimbo

Maneno ya Kiswahili yameweza kutumika pamoja na ya Kiingereza, kuonyenya uelewa zaidi ya lugha moja. Kutokana na tajriba walio nao wasanii hawa.


Mfano3 .Kibonzo # 1, # 2, #19, # 24, # 47.




Kibonzo hiki msemaji ametumia Kiswahili pamoja na Kiingereza. Anasema, ‘Naweza kuandikisha ‘ My DressMy Choice kama chama? Nimeona iko na wafuasi wengi.’ Wafuasi hao tunaona tu mabango ikiandikwa ‘ My dress My choice.




Katika kibonzo hiki ni wazi kuwa neno ambalo limefupishwa ni ‘sms’ ambalo kwa urefu ni Short Message Services.Vile vile tunapata kuwa yameandikwa kwa herufi ndogo ambalo linaleta ukiushi wa herufi kubwa kwa neno. ‘Sasa hii nitajibu kwa sheng ama kama sms. Mwanafunzi huyu hana uelewa wa yale ambayo anafanya katika mtihani huu.




Kibonzo hiki kinaonyesha wafu waliopiga kura wakati wa uchaguzi. Wasemezana wenyewe kwa wenyewe. Mare Hemu Died 2005, RIP, kikawa ni Rstless Mpiga kura Born 19…. DIED Dec 2007.



Kibonzo hiki nacho  kinaendeleza dhana ya uhuishi kwa kutumia msimbo. Wafu wanaongea,
‘ Ghost workers wenzangu, usajili unaoendelea unaweza tupeleka ritaya mapema’.
Mwenzanke akimshukuru, ‘ Asante Chairman kwa hiyo habari.’

**Hitimisho**

Sura hii, umeangazia masuala ya mitindo ya lugha ambayo imetumika katika vibonzo kwenye gazeti la *Taifa Leo.*  Matokeo ya uchanganuzi wa data kuhusu mitindo ya tamathali za lugha imejadiliwa , na ukiushi mbalimbali. Matokeo yanaonyesha kuwa wachoraji vibonzo wanaubunifu wa kujivunia. Baadhi ya mitindo tunayoangaza ni pamoja na ,jazanda, kanaya, chuku, kuchanganya msimbo, chuku, n.k. Matokeo yanaonyesha kuwa mbinu ya jazanda na kinaya  kama zimetumika kwa wingi.

## SURA YA TANO

## 5.0 MUHTASARI, MAPENDEKEZO, NA HITIMISHO

### Utangulizi

Sura hii ambayo ni ya mwisho katika utafiti huu. kazi imepangwa katika sura tano na katika sura hii tumetoa muhtasari wa sura hizo. Utathmini wa nadharia tete za utafiti ili kubainisha kama zinaunga mkono au zinapinga matokeo ya utafiti huu ulifanywa. Mwishowe tumetoa mapendekezo kwa watafiti wa baadaye.

### 5.1 Muhtasari

Ni muhimu kutambua kuwa utafiti huu ulinuia kutambua maudhui yaliyoko kwenye vibonzo pamoja na uainishaji wa mitindo ya lugha yaliyoko pale kwa kuyaoanisha na nadharia ya Utambulisho ya Giles. Tumechukua hatua kuziainisha jumbe katika maudhui mbalimbali kwa mfano, Siasa, Ufisadi, Ukosefu wa Usalama, Ukabila, Elimu, Uchumi na kazi. Maudhui haya yalitawala kwingi katika vibonzo vya gazeti la *Taifa Leo*. Pia, tumechunguza lugha inayopendelewa katika vibonzo na lugha ambazo zimejitokeza ni pamoja na Kswahili na Kiingereza.

Utafiti huu utachangia pakubwa katika kupanua mawazo ya wanajamii kuwa wazingatiivu katika vibonzo vinavyochorwa katika gazeti la *Taifa Leo*, maadamu huwa na jumbe nzito,kuhusu maisha ya wanajamii. Kwa hivyo, utafiti huu utakuwa kama kifungua machocha jamii. Matokeo ya uchanganuzi wa mitindo ya lugha, yatasaidia katika usomi wa kiisimu.

Katika sura ya kwanza tumeshughulikia utangulizi kwa jumla kuhusu tasnifu hii. Sura hii inatoa maelezo mwafaka kuhusu sura zilizotangualia kwa muhtasari tu. Hivyo basi inatupa uelewa wa tasnifu yote. Inaeleza jinsi ambavyo utafiti ulivyofanywa kama vile kutafuta gazeti la *Taifa Leo* kutoka kwa makavazi, kusajili yanayotufaa kwa utafiti kuhusu vibonzo.

Sura ya pili imeangazia vibonzo kwa kujadili historia yake na maendeleo yake na kuonyesha aina mbalimbali za vibonzo na mitindo mbalimbali za tamathali za lugha. Pia, tumejadili matumizi mbalimbali za lugha, na kuainisha jumbe kimaudhui katika makundi yafuatayo: Ufisadi, Siasa, Ukosefu wa Usalama, Ukabila, Elimu, Kazi na Uchumi katika vibonzo

kwenye *Taifa Leo.* Matokeo yanaonyesha kuwa maudhui ya Ufisadi na Siasa ndiyo yanayotawala katika vibonzo hivyo.

Katika sura ya nne tumefanya uchanganuzi wa mitindo ya lugha ambayo tumechunguza tamathali za lugha , pamoja na ukiushi. Imebainika kuwa tamathali za lugha kama Jazanda, Kinaya, Kejeli, Chuku zimetumika sana.

## 5.2 Changamoto za Utafiti.

Ni muhimu kutaja kuwa katika utafiti huu umekumbwa na changamoto kadhaa. Kwanza, nchini Kenya imefungwa katika gazeti moja tu la *Taifa Leo* linalochapishwa kwa lugha ya Taifa ambacho ni Kiswahili kwa hivyo maelezo ni kulingana na gazeti hili.. Aidha haikuwa rahisi kutafsiri vitabu vya marejeleo kwa kuwa nyingi zao ni za Kiingereza. Vile vile kuchanganua maelezo kwa takwimu ni sugu; kuzunguka maktabani hasa kwenye makavazi kusajili hayo gazeti la *Taifa Leo* hasa hizo za miaka ya 2013, na 2014 haikuwa ya kuliwaza . Katika Uchanganuzi wa data mtafiti alikumbwa na shida ya kupata kuwa vibonzo vingine vinabeba zaida ya maudhui moja kwa mfano vibonzo # 2, # 4, # 16, # 20 na vingine vilivyobeba zaidi ya mitindo moja. Kupata vitabu vya marejeleo kuhusu utafiti huu haukua rahisi kupata kwa sababu ilimlazimu mtafiti kusafiri hapa na kule kuvipata. Haikuwa rahisi kupiga chapa vibonzo hivyo vilivyokusanywa. Gharama ya utafiti pia ilikuwa juu kupiga chapa kazi yote wakati mwingine kazi kuzimia kabisa kutokana na kuliwa na virusi vya taraklishi. Hata hivyo , nimejizatiti na kufanikiwa kumaliza utafiti huu kwa wakati.

## 5.3 Mapendekezo

Katika utafiti huu, mtafiti alibanbanwa kwa upeo na mipaka yetu kwani kuna mambo mengi ya kutafitiwa katika eneo hili la vibonzo, na ambayo inatubidi kuyaacha nje. Kutokana na utafiti huu, tumegundua kuwa vibonzo vya magazeti yana jumbe nzito na kwa hivyo tungependelea:

a) Watafiti wachunguze vibonzo katika magazeti mengine, kama The Standard, The Star, Citizen X-News, n.k.

b) Watafiti watumie njia tofauti za utafiti kama mahojiano ili kupata maoni mbalimbali kutoka kwa wasomaji wa magazeti kuweza kupata maoni yao kuhusu vibonzo kwenye gazeti hilo.

c) Utafiti wa kulinganisha vibonzo vya magazeti tofauti tofauti ufanywe ili kubainisha iwapo kuna ufanano au ukinzano wowote kuhusu

d) Tafiti zifanywe kuchunguza sababu za tofauti za uchoraji katika vibonzo vya *Taifa Leo* na magazeti mengine.

e) Tafiti zifanywe kubainisha iwaapo vibonzo huwa ni miliki ya mtu binafsi au kazi ya jumuia, katika shirika la uchapishaji.

### 5.4 Hitimisho

Tuliorodhesha Nadharia tete tatu kwa ajili ya utafiti huu. Nadharia tete yetu ya kwanza ilidai kuwa maudhui kuhusu ufisadi na siasa yanatawala katika vibonzo hivyo. Matokeo yanaonyesha kuwa ufisadi na siasa ndiyo maudhui tawala , hivyo basi nadharia tete hii ni ya ukweli kabisa.

Uchanganuzi huu ilihusu lugha inayopendelewa sana katika vibonzo umedhihirisha kuwa lugha ya Kiswahili ndiyo inayopendelewa. Nadharia tete ya pili si ya ukweli kwani tulichukulia kuwa sheng ndio lugha pendelewa kwa vile asilimia kubwa ya jamii hii huathiriwa na sheng. Hata hivyo, suala la kuchanya msimbo limejitokeza kutokana na hali ya wingilugha katika mazingira wanamo chorea wasanii.

Matokeo ya uchanganuzi wa mitindo ya lugha yanakubaliana na nadharia tete ya tatu kwani matumizi ya tamathali za lugha , inatawala sana katika vibonzo hivyo.

### 5.5 Baadhi ya Istilahi zilizotumika

| | |
|---|---|
| Acronimu | Acronym |
| Filamu | Film |
| Jamiilugha | Speech community |
| Katiba | Constitution |
| Kibonzo | Cartoon |
| Lugha pendelewa | Preffered language |
| Lugha rasmi | Official language |
| Lugha vipindi | Slang |
| Lugha ya Taifa | National language |
| Makutano | Convergence |
| Miktadha ya Kimaikro | Micro context |
| Miktadha ya Kimakro | Macro context |
| Mwachano | Divergence |
| Tahajia | Spelling |
| Uasilia | Originality |
| Ubunifu | Creativity |
| Ufupishaji maneno | Abbreviation |
| Ugatuzi | Devolution |
| Ujihusishaji | Accomodation |
| Ukiushi | Deviation |
| Utambulisho | Identity |
| Wingilugha | Multy lingual |

## MAREJELEO


Adegbija, E. (1999) "*Titbits on Discourse Analysis and Pragmatics*" in the Englisg and Literature in English. An Introduction . I lovin, Department of Modern European Languages, Unilovin.

Angumbi, P.F. (2011) *'Style shifting in spoken communication in cartoons in Standard News paper in Kenya'.* Maseno University: Unpublished M.A Thesis.

Anderson, J. A & Meyer, T.P (1988). *Mediated Communication : A Social interaction perspective*. Newsbury Park, CA: Sage

Ahyana, N. L (2011). Implicature Used in the Headline News of I ndonesia. *This Morning program in Metro T.V.* Univesita IslamNegeri. Malay.

Askew, K. (2003*) Performing the Nation*: *Swahili Music and Cultural Politics*. Dar es Salaam; Kapsel

Bateman, T.S & Zeithaml C.P(1993). *Management Function and Strategy, 2nd ed.* Boston, Massachussetts: Richard D.irw, inc.

Beck, R. M. (1999) *Comic in Swahili or Swahili Comic?* http: // www,vmcaa,nl// bongotoons/ engels/pages/strip figuren.htm. Accessed 22 .07.2015

Beez, J. (2003) 'They are Crazy these Swahili-Komredi Kipepe in the footsteps of Asterix : Globalisation in East Africa Comics'.*Internatinal Journal of Comic Art* ( 5;pp 95-114).

Beez, J. (2004) ' Katuni za Miujiza'; Fantastic Comics from East Africa *' International Journal of Comic Art*. (6: pp 77-95).

Bichanga,W.N. & Aberi, G. (2012) Kenyan Media Discourse: ACritical Analysis of News Headlines on 2007 Election Campaigns. Journal of Education and Social Sciences, Nairobi:Mount Kenya University.

Bohl, A(1997).*Guide to Cartooning*. Gretna ; Pelican Publishing.

Canadian International Development Agency Kenya. (2008). *Kenya Media Sector analysis report.* Nairpb: ABC.

Condit, C.( 2001). An exploratory study of the impact of news headlines on genetic determinism. *Science Commununiaction*, London: London.

Chris, H. & Patrick, M .(2013*), Devolution in K enya : Opportunities and Challenges.*

Coleman et al (2009) Agenda Setting. In Kari Wahl- Johgensen & Thomas Hanitzsh, *The Handbook of Journalism Studies*.New York Routledge (pp 149-160)

David, A. (1995) Guardian pocket *Cartoonist with a skeptically humanist view of the news* .Cambrige University Press.

Dijk, TV (1998). *Political Discourse and Ideologhy. Barcelona* : University of Amsterdam.

Fairclough, N. (2004) *Discourse Analysis.* London: Routledge.

Feldman , O. (2005) *Talking Polics in Japan Today*. Brighton Sussex  Academics Press

Friedrich, E. F (2001). *Art in Politic- Sanaa katika Siasa. The first African Competition Carricatures and Cartoons*. Dar es Salaam: Friedrich Ebert Stiftung

Fox , J & Hoffman , W. (2011) *The Differentiated Instruction Book of Lists*.Hoboken: John Wiley & Sons.

Gikonyo, W. (1986). 'Comics and Comics Strips in the Mass Media Kenya'. *In Comics  and Visual Culture :* Research Studies from ten Countries, edited by Alphons Silbermann & H.D. Dyroff, (pp 183-191). Munchen; Saur.

Giles, H. (1982).*Communication Accomodation Theory*.New York: Cambrige University press.

Giles, H .& Coupland, N. (1991) *‘ Accomodation Theory: Communication contex and consequence* “ in Giles, Howard; Coupland, Justine Contex of Accomodatin .New York, Cambrige University Press.

Griffin .E (200) *A first look at Communication Theory* 7th ed. New York: Mc Graw- Hill

Harvey , R.C. (1994) .*The Art of Funnies :An Aesthetic History* .University of Missisippi Press.

Grice, H.P. ( 1989). *Studies in the way of words*. Massachusetts : Havard University Press.
Hess, S. & Northrop, S. (2011) *American Political Cartoons : The Evolution of a National Identity , 1754-2010*. Montgomery: Elliot & Clark.

Hoggarth . W. (1989) *Hogarths Graphics* 3rd edition, London .# 43.

Ingutia, A. A. (2012*) Lexico-grammatical Analysis of Newspapers editorials cartoons in the run-up to the 2007 general elections in Kenya: perception and attitude in the Standard and daily Nation*, M.A Thesis University of Nairobi Unpublished.

Johnson, R.B & Onwuebuzie, A.J (2004) *Mixed Methods Research*. A research Paradgm.Who’s time has come Educational Research vol 33 no7 pg 14-26.

Kamusi ya Karne ya 21.*Kamusi ya Kiswahili*. Longhorn Publishers expanding minds

Kiriara, J. (1995) Literature in Kenya:the influences and effects of publishing.Katika: Kwadzo Senanu & Drid Williams (eds) *Creative Use of Language*. Nairobi : The Jomo Kenyatta Foundation.

Kei .K.J. (2002) ‘Nafasi ya Kiswahili Katika Ujenzi wa jamii Mpya ya Afrika Mashariki’, ‘Nordic Journal of African Studies, ( pp 185-197). West port, CT: Praeger.

Kumar, R. (2011). Research Methodology: A step-by-step guide for beginners. London : SAGE.

Kunzle, D (1973). The Early Comic Strip: Narrative Strips and Picture Stories in the European Broadsheet from C1450 to 1825. Berkely. University of Calfornia  Press.

Lent, J.A. (1996*). Comic Art in Africa , Asia, Australia, and Latin America* : *A comprehensive International bibliography*. West port: Greenwood press.

Lordan, E. J. (2006). Politics, Ink : How American Cartoonists Skewer Politicians from King George iii to George Dubya. Oxford Bowman & Little field.

Mathooko, M. (2007) Isimu jamii; *Misingi na Nadharia* Nairobi:Njogu Books.

Maloba, W. (1992) The Media and Mau Mau : Kenyan Nationalism and colonial propaganda. In Beverly G. Hawk 9 Ed), Africas Media image. New York : Praeger.

Mbaabu, I. & Kipande , N.(2003). Sheng-English Dictionary : Deciphering East Africas Underworld Language. Dar es Salaam. TUKI

McClouds, S. (1993). Understanding Comics: The invisible Art. Northampton ; Kitchen Sink Press.

McCombs, M. (2004*) Settling the Agenda : The Mass Media and Public Opinion*. Malden : Blackwell Publishing.

McLeod .S.A.  (2008) *Simply Psychology*. Online [http// www.simplypsychology.org qualitative-quatitative.htm ( accessed 22nd April 2015]

Mugenda, O.M & Mugenda ,G. A. (1999*) Research Methods: quantitative and Qualitative Approaches.* Nairobi ; Acts Press.

Musamali, C.O. (2012 ) *Ufasiri Kipragmatiki wa wakazi wa eneo la msitu kuhusu Diskosi katika Gazeti la Taifa Leo*.M.A Thesis Maseno Univesity Unpublished.

Njogu, K & Chimera (1999) Ufundishwa Fasihi : Nadharia na Mbinu.Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Njoku, U. K . (2011) *A pragmatic Study of some selected political Posters*. University of Ilrin. Nigeria.

Obonyo, L. ( 2004) ‘ Cartoonists in Kenya : Past Present and Future’.International Journal of Comic Art ( 6 pp 96-116).

Ogechi, N.O. (2002) *Mbinu za Mawasiliano Kwa Kiswahili*. Moi University Press.

Pride, J.B. (1971 ) *The social meaning of Language*.London: Oxford University Press.

Sterlin, C. (2009) *Encyclopedea of Journalism*.Thousa Oaks: Sage Publication, inc, pp253-261.

*Taifa Leo*. Nation Media Group Limited.

Reah, D. (1998). *The Language of News Papers.* London & NewYork: Routledge.

Republic of Kenya (2010). *Constitution of the Republic of Kenya*, National Council for Law reporting : Nairobi. Government Printing Press.

TUKI (2002) *Kamusi ya Kiingereza-Kiswahili*. Institute of Kiswahili Research University of Dar es salaam.

TUKI (2000). Swahili – English Dictionary . Dar es Salaam : Taasisi ya Uchunguzi wa Kisawahili.


Transparency International Kenya-*Devolution Handbook* (2014). Government Printing Press.

, L.H and Richard .W. (2010) Communication Accommodation Theory. *Introducing Accomodation Theory*: Analysis and Application 4th ed.New York Mc Graw-Hill.

World Bank. (2012). *Devolution without Disruption* . Pathways to a Successful New Kenya: Nairobi : World Bank.www-wsp.org

Stavall, J. G. (2002). *Writing for the Mass Media*. Boston: Allyn and Bacon.

**VIAMBATISHO**




1





2





3


TAIFA LEO 11
Ijumaa, Julai 26, 2013
Jihadhari na wanaotumia kabila kutafuta kura
KABILA
©IGAH

4


TAIFA JUMAPILI 11
Julai 28, 2013
UKABILA
MITANDAO
©IGAH


5



TAIFA LEO 11
Jumamosi, Julai 6, 2013
Madam, ile bomu sisi huambiwa tutafute hukaaje?
©IGAH

6

7


TAIFA LEO 11
Alhamisi, Agosti 1, 2013
Tafadhali niimbie wimbo wa Taifa
Solidarity forever, Solidarity forever....
Music
©IGAH

8

TAIFA LEO 11
Jumatatu, Juni 24, 2013
Mtihani wa leo sio mgumu
VYUO
©IGAH

9

TAIFA LEO 11
Jumatano, Oktoba 29, 2014
Subiri. Bado tunangojea pesa kutoka kwa Serikali kuu
PROJECT
SERIKALI ZA KAUNTI
©IGAH


TAIFA LEO 11
Jumatatu, Oktoba 13, 2014
Mheshimiwa, naona katika bajeti ya Kaunti, tutenge pesa za kuwanyamazisha MCA
GAVANA
©IGAH


10


TAIFA LEO 11
Jumatano, Agosti 21, 2013
Najivunia kuwa Mkenya
Michezo imeisha. Uhusiano wetu umeisha!
SIASA
©IGAH


11


TAIFA LEO
Jumatatu, Novemba 3, 2014
Sasa tutafutiwe hata kama ni masoja wa kutulinda 24 /7
©IGAH

12


TAIFA LEO 11
Jumanne, Agosti 13, 2013
Nitakumaliza
UCHOCHEZI
GK
UKABILA
©IGAH

13


TAIFA LEO 11
Jumatano, Oktoba 2, 2013
Twaomba yeyote aliye na habari kuhusu uhalifu ajitokeze
WESTGATE
Uchunguzi wa kina utafanywa kuhusiana na suala hili
WESTGATE
WESTGATE
Atakayepatikana na hatia, atahukumiwa
©IGAH

14


TAIFA LEO 11
Jumamosi, Agosti 24, 2013
KSHS
Karibia kwa Mpesa. Natuma saa hii
ATM
KOSA BARABARANI
©IGA


15


TAIFA LEO 11
Jumatatu, Agosti 26, 2013
Naunga mkono hoja ya kura ya maoni kuwa hela za Kaunti ziongezwe
...ili tupate za kuiba
©IGAH


16


TAIFA LEO 11
Jumanne, Julai 30, 2013
HISIA KWA MITANDAO
©IGAH


17


TAIFA LEO 11
Alhamisi, Julai 11, 2013
UFISADI
KIINUA MGONGO
HONGO
MLUNGULA
KITU KIDOGO
Najivunia kuwa Mkenya
©IGAH

18


TAIFA LEO 11
Jumatatu, Julai 8, 2013
Ulipigia kura wapi?
Tshhhh! Nyamaza.Sitaki kugunduliwa
????
Mare Hemu
Died 2005
RIP
Restless
MPIGA KURA
BORN 19.....
DIED Dec 2007
©IGAH


19


TAIFA LEO 11
Alhamisi, Agosti 29, 2013
MFUMUKO WA BEI
USALAMA
NJAA
IDP'S
UKOSEFU WA KAZI
SIASA
Nitajivunia kuwa Mkenya?
©IGAH

20


TAIFA LEO 11
Jumatatu, Agosti 5, 2013
Nikilemewa, nitalaumu mgomo wa walimu
MITIHANI
©IGAH

21


TAIFA JUMAPILI 11
Agosti 4, 2013
TAASISI ZA ELIMU
JOBS
©IGAH

22


TAIFA JUMAPILI 11
Agosti 25, 2013
Tunaishi kama ndugu na dada
UKABILA
©IGAH


23


TAIFA JUMAPILI 11
Oktoba 13, 2013
Sasa hii nitajibu kwa sheng ama kama sms
MITIHANI
©IGAH


24


TAIFA LEO 11
Alhamisi, Oktoba 3, 2013
VIPI MTU WANGU?
TUOMBEE AMANI NCHINI
WAKENYA
©IGAH

25


TAIFA LEO 11
Jumamosi, Novemba 2, 2013
WANA-HABARI
MEDIA BILL
©IGAH


26


TAIFA LEO 11
matatu, Julai 29, 2013
KENYA @50
©IGAH

27


TAIFA LEO 11
Jumatatu, Septemba 8, 2014
GAVANA
MP
MCA
PESA MASHINANI
PESA KWA WANJIKU....
©IGAH

28


TAIFA LEO 11
Septemba 30, 2014
ZZZZZZZ
MKENYA
Niamshwe hizo pesa zikifika hapa mashinani
©IGAH

29


TAIFA LEO 11
Alhamisi, Julai 4, 2013
These premises are under CCTV Surveillance
PRO-SCAN II
Tunatafuta silaha zote kali kali
©IGAH


30


TAIFA LEO 11
Jumatano, Julai 3, 2013
SERIKALI
MKATABA
Sahihi
WALIMU
©IGAH

31


TAIFA LEO 11
Jumanne, Novemba 5, 2013
Mtoto akililia wembe mpe!
©IGAH


32


TAIFA LEO 11
Ijumaa, Oktoba 24, 2014
Mashinani ni popote. Hata hapa tulipo
PESA MASHINANI
Hilo ni wazo nzuri. Nipe zangu
©IGAH


33


TAIFA LEO 11
Jumanne, Oktoba 14, 2014
Mheshimiwa, msimamo wako kwa Vision 2030?
Najua tu kuhusu vision ya miaka ya uchaguzi
©IGAH

34


TAIFA LEO 11
SERIKALI VS WANAHABARI
©IGAH


35


TAIFA LEO 11
Jumanne, Oktoba 8, 2013
AJIRA
HAKUNA KAZI
UGAIDI
Karibu ndani
alshabaab was here
©IGAH


36


TAIFA LEO 11
Alhamisi, Juni 27, 2013
Kama sio mgomo...
E
©IGAH


37


TAIFA LEO 11
Jumamosi, Julai 27, 2013
TUHUBIRI AMANI
UKABILA
©IGAH


38


TAIFA LEO 11
Jumanne, Oktoba 15, 2013
UGAIDI
SERIKALI
©IGAH


39


TAIFA LEO 11
Jumatano, Agosti 28, 2013
Twaomba yeyote aliye na habari kuhusu uhalifu ajitokeze
Uchunguzi wa kina utafanywa kuhusiana na suala hili
Atakayepatikana na hatia, atahukumiwa
©IGAH

40


TAIFA LEO 11
Jumatano, Septemba 18, 2013
Una habari kuwa watu 5,048 watapigwa kalamu?
Siogopi. Ghost wokers ndio wataenda.
BARAZA LA JIJI


41


TAIFA LEO
Ijumaa, Julai 19, 2013
11
Najivunia kuwa Mkenya
ULAFI
ULAFI
RUSHWA
ULAFI
HONGO
KIINUA MGONGO

42


TAIFA LEO
11
NAFASI ZA KAZI SAUDI ARABIA
CV
©IGAH


43


TAIFA LEO
Jumanne, Julai 23, 2013
Ili tuweze kuwahudumia wananchi vizuri...
GAVANA
Tuongezewe pesa kwa bajeti zetu
TAMAA
©IGAH

44


TAIFA LEO
Jumamosi, Agosti 3, 2013
11
JAMII
WIVU
SHAKA
UKABILA
CHUKI
HILA
©IGAH

45


TAIFA LEO
Jumanne, Septemba 16, 2014
11
MAGAVANA
BUNGE
HAZINA YA KITAIFA
©IGAH


46


TAIFA LEO
Alhamisi, Septemba 4, 2014
11
Ghost workers wenzangu, usajili unaoendelea unaweza tupeleka ritaya mapema
Asante Chairman kwa hiyo habari
R.I.P
R.I.P
©IGAH

47


TAIFA JUMAPILI
Septemba 7, 2014
11
Pamoja tuangamize wezi wa kuku
UFISADI
©IGAH

48


TAIFA LEO
Ijumaa, Oktoba 11, 2013
11
HATARI ZA KUJIVUNIA KUWA MKENYA KWA......
...KUISHI,
....KUSAFIRI
....KULA
PSV
KWIK
FAST FOODS
TAKE AWAY
©IGAH

49


TAIFA LEO
Alhamisi, Juni 20, 2013
11
MSAJILI
Sio vitambulisho, tunataka pesa za Hazina ya vijana
©IGAH

50